**Benki** ya NMB yaongeza mapato kwa asilimia 20, yapata faida ya bil. 134/-

UKURASA 3



**Watalii** 550 kutoka Israel kuwasili nchini kutembelea vivutio

UKURASA 7


Nipashe Spotika
KLABU ANAZOWEZA KUTUA KOULIBALY
ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Agosti 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580660

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Chanjo corona milioni 11 yaja

## SERIKALI yasema waliochanjwa hawajapata madhara...

*Endelea ukurasa 2*



Wananchi wakiwa katika foleni ya kuchukua namba za kuchoma chanjo ya corona katika jengo la Mikutano la Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## NSSF sasa kuwekeza kilimo cha mkonge

UKURASA 3



## Uamuzi mpya tozo ya miamala ya simu waiva

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA, AZAM ZAFUNIKA USAJILI, SIMBA KIMYA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Chanjo ya corona milioni 11 yaja nchini

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema dozi nyingine milioni 11 ya chanjo ya Uviko-19 inatarajiwa kuletwa nchini wakati wowote.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Msemaji na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO), Gerson Msigwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam.

Msigwa alisema uhitaji wa chanjo ya Uviko-19 nchini ni kufikia asilimia 60 ya Watanzania wote na dozi hiyo milioni 11 ikiletwa nchini itakuwa imefikia asilimia 20 pekee ya mahitaji.

"Kuna dozi milioni 11 tunazotarajia kuzipata kutoka Covax Facility na tukizipata hizi tutakuwa tumefikisha asilimia 20 tu ya mahitaji. Nchi yetu imejiwekea mipango tupate kama asilimia 60 hivi ya mahitaji, kwa hiyo tuna kazi ya kutafuta nyingine asilimia 40 ambayo wataalamu wanatueleza kwamba tukitoa chanjo kwa asilimia 60 ya Watanzania tutakuwa tumejihakikishia kukata maambukizi ya huu ugonjwa ambao kwa sasa unasababisha madhara makubwa," alisema Msigwa.

"Chanjo zitakuja nyingi na tayari chanjo kama tano, sita, saba hivi zimetambuliwa na kukaguliwa na zitakuja kwa awamu kwa sababu zinahitaji kuhifadhiwa vizuri, na hizi dozi milioni 11 zinaweza kuletwa ndani ya wiki mbili au tatu hivi." Aliwasisitiza wananchi kusikiliza elimu inayotolewa na wataalamu na kuachana na maneno ya upotoshaji yanayotolewa na baadhi ya watu kupitia mitandao ya kijamii kuhusu chanjo hiyo.

"Serikali inapenda kuwasisitiza wananchi kuwasikiliza wataalamu wa afya, tatizo tulilonalo sasa hivi kila mmoja amejivalisha utaalamu, tusiwasikilize wasio na utaalamu," alisisitiza Msigwa.

"Hakuna madhara kwa waliochanja na mpaka sasa msimamo wa serikali bado chanjo ni hiari, kwa hiyo niombe wapotoshaji waache wananchi waamue, wasiwapotoshe."

Msigwa alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kupotosha taarifa za chanjo.

Tayari Tanzania imepokea chanjo 1,058,400 ya Uviko-19 aina ya Johnson Johnson ambayo ilitoka Serikali ya Marekani kupitia Covax Facility. Wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan, aliizindua chanjo hiyo na kuchanjwa pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali waliokuwapo katika tukio hilo la uzinduzi.

Dozi hiyo tayari imeanza kusambazwa katika mikoa mbalimbali na leo au Agosti 5 wananchi watakaohiari wataanza kuchanjwa. Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, vituo takribani 550 vitatumika kutoa huduma hiyo ya chanjo.

Masharti ambayo yamewekwa na wizara hiyo kwa wanaohitaji kupata chanjo hiyo ni pamoja na kutakiwa kujisajili kwa kutumia mtandao wa ndani ya simu au kompyuta, kutoa kipaumbele kwa makundi yenye uhitaji mkubwa ikiwamo watumishi wa sekta ya afya, watu wazima kuanzia umri wa miaka 50 na kuendelea na wenye magonjwa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizindua Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Busokelo, mkoani Mbeya. Wengine kutoka kushoto ni Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako na kulia ni Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete. **PICHA: PMO**

## Samia kwenda Rwanda leo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, leo anatarajia kuanza ziara rasmi ya kiserikali ya siku mbili nchini Rwanda kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo, Paul Kagame.

Taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu iliyotolewa jana, ikulu jijini Dar es Salaam ilieleza kuwa akiwa nchini humo, Rais Samia pamoja na mambo mengine, atafanya mazungumzo rasmi na mwenyeji wake Rais Kagame, kisha atashuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano na kuzungumza na vyombo vya habari.

Ziara hiyo inalenga kuimarisha zaidi uhusiano na ushirikiano kati ya Rwanda na Tanzania.

Hii ni ziara yake ya nne nje ya nchi tangu aingie madarakani Machi mwaka huu. Ziara ya kwanza aliifanya Uganda kusaini mkataba na Rais Yoweri Museveni wa bomba la mafuta kutoka Hoina hadi jijini Tanga. Ziara ya pili aliifanya Kenya kwa mwaliko wa Rais Uhuru Kenyatta na ya tatu aliifanya mwezi uliopita nchini Burundi.

Ziara ya Rwanda inamwezesha kuzitembelea nchi tano kati ya sita wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Mbali na nchi hizo nyingine ni Sudan Kusini, ambayo ni mwanachama mpya.

Rais Samia pia alikwenda Msumbiji safari ambayo hata hivyo, haikuwa ya ziara rasmi, ambapo alihudhuria mkutano wa dharura wa viongozi wakuu wa nchi na serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

# Uamuzi mpya tozo miamala ya simu waiva

**Na Elizabeth Zaya**

UAMUZI mpya kuhusu tozo ya miamala ya simu unatarajiwa kutolewa wakati wowote.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO), Gerson Msigwa, alisema Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, waliwasilisha taarifa ya mapendekezo yao kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, juzi.

"Jana (juzi), Waziri wa Fedha na Mipango na Waziri Mawasiliano, waliwasilisha taarifa ya mapendekezo ya tozo za miamala ambayo wameyatoa juu ya maelekezo waliyoagizwa na Rais Samia ya kufanyia kazi madai ya wananchi kuhusu miamala ya tozo," alisema Msigwa.

"Tayari Waziri Mkuu ametoa maelekezo mengine ya namna ya kwenda kurekebisha na kuiweka vizuri taarifa hiyo, sitakuwa na majibu leo (jana) juu ya nini kimeamuliwa, lakini wakati wowote serikali itakuja na majibu na maelezo. Tusubiri taarifa itakayotolewa wakati wowote kuhusu tozo hizo za miamala."

Julai 19, mwaka huu, Dk. Mwigulu alitoa taarifa kwa umma kwamba serikali imesikia maoni ya wananchi kuhusu tozo hizo za miamala ya simu, na kwamba viongozi wakuu wameagiza kuitishwa kwa kikao cha kujadili suala hilo.

Dk. Mwigulu alitoa kauli hiyo baada ya siku chache mwezi uliopita kuanza rasmi kwa utekelezaji wa bajeti ya serikali ya 2021/2022 ikiwamo kuanza rasmi kwa tozo za miamala zilizosababisha kuibuka kwa mjadala mkubwa kutoka kwa wananchi kuhusu tozo hizo.

Mjadala ulioibuka kwa wananchi ni kuhusu kiwango kikubwa cha tozo hizo za miamala kinachotozwa, japokuwa serikali ilitolea ufafanuzi sababu za kuweka tozo hizo.

"Nitoe rai kwa wananchi kwamba serikali imesikia maoni yote yaliyotolewa na wananchi na tumeendelea kuyafanyia kazi," alisema Dk. Mwigulu Julai 19, mwaka huu.

"Viongozi wetu wakuu, wamesikia maoni yote yaliyotolewa na wananchi. Rais naye ameguswa na jambo hili, amesikia maoni ya Watanzania wote na alishatolea maelekezo kwamba tuyafanyie kazi haya ambayo wananchi wanayatoa."

"Tayari Waziri Mkuu ameitisha kikao ambacho kitafanyika kesho (Julai 20) ili kuendelea kupitia masuala haya haya. Nitoe rai kwa wananchi kuwa watulivu kwenye jambo hili, tutaendelea kuelezea na kutolea ufafanuzi kwenye kila maeneo ambayo yanahitaji ufafanuzi na tutachukua hatua kwenye yale maeneo ambayo yanayohitaji kuchukuliwa hatua ili ujenzi wa taifa letu uendelee kama ambavyo wananchi wetu wamekuwa na shauku kubwa ya ujenzi wa taifa letu kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi yetu."

Akitoa taarifa hiyo Julai 19, Dk. Mwigulu alisema mambo ambayo ni ya kisheria yanatakiwa kuheshimiwa, lakini mambo ambayo ni ya kikanuni yatafanyiwa kazi kama ambavyo wameagizwa na viongozi wakuu wa nchi.

"Mambo ambayo ni ya kisheria, sheria za nchi zinatakiwa kuheshimiwa, lakini mambo ambayo ni ya kikanuni na ambayo yanahitaji uelimishwaji tutaendelea kufafanua, lakini yale ambayo ni ya kikanuni na yanahitaji kufanyiwa kazi kama ambavyo viongozi wetu wametuagiza tutayafanyia kazi," alisema Dk. Mwigulu.

HABARI KITAIFA

# NSSF kuwekeza kwenye kilimo cha mkonge

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wadhamini ya Mkufo wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Balozi Ali Iddi Siwa, amesema sheria iliyoanzisha NSSF inawaruhusu kuingia katika uwekezaji na wanataka kutengeneza fedha kupitia kilimo cha mkonge.

NSSF ilianzisha kampuni tanzu ya Sisalana Tanzania Limited, kwa ajili ya kusimamia shughuli zote zilizokuwa zinafanywa na Kampuni ya Katani katika usindikaji wa mkonge, NSSF ilichukua baadhi ya mali za kampuni hiyo ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo uliotolewa na shirika hilo baada ya kushindwa kurejesha mkopo huo. Lengo la NSSF ni kurejesha fedha zake ambazo ni za wanachama wake.

Alisema kampuni ya Sisalana imepewa jukumu la kuendesha korona tano (mashine za kuchakata mkonge) kwa lengo la kurudisha fedha ambazo NSSF ilikopesha kampuni ya Katani Limited.

"Kwa hiyo Sisalana imeingia ili iweze kurejesha fedha za wanachama na inaendesha shughuli za biashara hiyo kwa kushirikiana na AMCOS (Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Mazao), ambapo kazi yake kubwa ni kuchakata majani ya katani ili AMCOS ziweze kuuza brash ambayo inaitwa singa na sisi tunapata tozo kutokana na kuchakata huko," alisema.

Alibainisha kuwa NSSF kupitia Sisalana inataka itanuke zaidi katika biashara ya mkonge na tayari wana mikakati ya kuendelea mbele na inaiunga mkono na wanasimamia miradi ili iwe inafuata taratibu na kanuni za uwekezaji ambazo zinatawala Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Balozi Siwa alisema biashara ya mkonge siku za mbele itatanuka zaidi na Sisalana inataka itengeneze fedha ili iwe na uwezo mkubwa wa kuzalisha.

Aliwaomba wadau wenzao ambao ni AMCOS waendelee kujenga ushirikiano mzuri ambao tayari umeshaanza kukomaa kwa kuwa lengo lao ifike mahali ikizungumzwa habari ya mkonge Mkoa wa Tanga uwe unaizungumza Sisalana nyuma yake chini ya NSSF.

Balozi Siwa alisema kutokana na halisi hiyo ndio maana wameingia katika biashara ya mkonge na wanataka biashara hiyo iwe na maana katika kutunisha NSSF ili iwe na uwezo mkubwa wa kulipa pensheni kwa wanachama.

Alisema kupitia ushirikiano huo kuna wadau watatu ambao ni serikali na Bodi ya Mkonge ambayo kazi yake ni kusimamia sera na kutoa miongozo, AMCOS ambao ni vyama vya ushirika vya wakulima ambavyo vinavyozalisha mkonge na Sisalana ambaye ni mdau wa tatu.

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basilla Mwanukuzi, alisema serikali imedhamiria kukuza uzalishaji wa mkonge kwa kuwa ni zao la kimkakati, lengo ni kuhakikisha wakulima wanaufaika na zao hilo kupitia vyama vya ushirika.

Alisema Sisalana ndio mkombozi wa kulikomboa zao la mkonge nal itakuwa chanzo kikubwa cha kuwawezesha wakulima kununua na kuchakata katani yao.

Shedrack Lugendo, ni Mwenyekiti wa Magunga AMCOS, alisema wakulima wadogo wa mkonge wana mwamko mkubwa baada ya serikali kuwaona na AMCOS kuwapa uwezo wa kujiuzia wenyewe mazao yao.

Alisema sasa uzalishaji umekuwa mkubwa na mashamba mengi ambayo yalikuwa yamekufa wakulima wake wanayafufua baada ya kampuni ya Sisalana kuingia.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima (kulia), akitazama mkonge uliochakatwa katika Kiwanda cha Mwelya kilichoko wilayani Korogwe mkoani Tanga, kinachomilikiwa na NSSF kupitia kampuni tanzu ya Sisalana. Katikati ni Giliad Kisaka, Mshauri na Mtaalamu wa Mkonge na mashine za uzalishaji wa zao hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NMB yaongeza faida hadi bil. 134/-

**Na Elizabeth Zaya**



BENKI ya NMB, imesema katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka huu, imeongeza faida hadi kufikia Sh.bilioni 134 ikilinganishwa na Sh.bilioni 94 ya kipindi kama hicho mwaka jana.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna, alisema faida hiyo imetokana na ufanisi wa utendaji kazi uliochangia ongezeko la biashara na miamala, udhibiti wa gharama za uendeshaji na ubora wa mikopo inayotolewa.

"Mapato ya benki yameongezeka kwa asilimia 20 hadi kufikia Sh. bilioni 463 katika kipindi kilichomalizikia Juni mwaka huu, ikilinganishwa na Sh. bilioni 387 zilizopatikana katika kipindi kama hicho mwaka jana. Mapato haya yamechangiwa na ongezeko la mikopo kwa wateja na uwekezaji kwenye hati fungani za serikali," alisema Zaipuna.

"Pia, mapato yasiyotokana na riba yameongezeka kwa asilimia 17 hadi kufikia Sh.bilioni 140 ikilinganishwa na Sh. bilioni 119 ya kipindi kama hicho mwaka jana. Ongezeko la mapato yasiyo ya riba yalichangiwa na ongezeko la miamala ya kibenki kutokana na huduma nzuri zinazotolewa na benki, mahusiano mazuri na wateja, na uwekezaji katika mifumo ya kidigitali."

Alisema katika kipindi hicho cha nusu ya kwanza ya mwaka huu, uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato halisi umeimarika mpaka kufikia asilimia 47 kutoka asilimia 56 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Alisema katika kipindi hicho, ubora wa mali za benki hiyo uliimarika kutokana na mikakati ya kuimarisha mikopo ya benki na kwamba uwiano wa mikopo chechefu uliimarika hadi asilimia 4.3 kutoka asilimia 6.9 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Zaipuna alisema mikopo ilikuwa kwa asilimia 11 hadi kufikia Sh. trilioni 4.2 kufikia mwisho wa Juni mwaka huu ukilinganisha na Sh. trilioni nne(4) katika kipindi kama hicho mwaka jana.

"Amana za wateja zilikuwa kwa asilimia nane(8) hadi kufikia Sh. trilioni 5.8 ikilinganishwa na Sh. trilioni 5.5 katika kipindi kama hiki mwaka jana, hii ikionyesha mazingira mazuri yaliyowekwa na benki katika uhusiano wake na wateja. Katika kipindi hiki mali za benki zimeongezeka kwa asilimia sita (6) hadi kufikia Sh. trilioni 7.6 ikilinganishwa na Sh. trilioni 7.2 katika kipindi kama hiki mwaka jana.

# Makongamano yamwibua Tundu Lissu

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Tanzania Bara, Tundu Lissu, ameeleza kushangazwa na kukamatwa kwa Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, wakati akijiandaa na kongamano la Katiba mpya jijini Mwanza.

Lissu ambaye yupo ughaibuni kwa sasa, ameyasema hayo katika majadiliano yake ya mtandaoni kuhusiana na hali ya kisiasa nchini akidai kuwa awali vyama vya upinzani vilizuiwa kufanya mikutano ya hadhara, huku serikali ikiruhusu mikutano ya ndani na makongamano ambayo hata hivyo, sasa wamezuliwa kufanya.

"Tumefanya kile tulichoambiwa tunaruhusiwa kufanya, sasa inaonekana hatuna adabu, kitu pekee wanachokitaka ni sisi tuzibe midomo yetu," alisema Lissu.

Mbowe aliyekamatwa jijini Mwanza Julai 21, mwaka huu wakati akijiandaa kushiriki katika ongamano la Katiba mpya lililoandaliwa na Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA). Mbowe ameshafikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka ya ugaidi na njama za kutaka kuua viongozi wa serikali.

Juzi Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, alitangaza maazimio ya chama hicho kuhusiana na suala la kukamatwa kwa Mbowe, akitangaza Alhamisi kama siku ya wafuasi wa chama hicho kujitokeza kupinga kushtakiwa kwa mwenyekiti huyo kwa njia mbalimbali ikiwamo maandamano ya amani nchi nzima.

Mikusanyiko ikiwamo makongamano imepigwa marufuku na baadhi ya wakuu wa mikoa ikiwamo katika mkoa wa Mwanza na Mbeya kwa kile kilichoelezwa kuepuka kusambaa kwa maambukizi ya virusi vya corona, wakisisitiza kuchukua hatua kali za kisheria kwa yeyote atakayekiuka katazo hilo.

"Sisi tunazuia maambukizi, tunataka vifaa vya kuwasaidia madaktari kuwahudumia wananchi vizuri, lakini kuna watu wanataka mikusanyiko na mikusanyiko yoyote lazima iwe na kibali ...sasa wewe jichanganye huko tukikufurumusha usije ukalalamika," alionya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

FADHILI R. KAMETA anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj liyokuwa na namba ya usajili **MC 388 CRF** na chasis namba MD6M14PA8L4B10047 na engine namba **AK4BL4611022.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/370489/2021**

116388002

KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

HAPPY EBEAT MANGULA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 692 DHY** yenye chasis namba **SXA160029523.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/313959/2021**

116387902

# TANGAZO

## THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY

The Mwalimu Nyerere Memorial Academy (MNMA) invites all qualified Tanzanians and None Tanzanians to apply for Basic Technician Certificate, Ordinary Diploma, Bachelor Degree and Master Degree at Dar es Salaam Main Campus, Karume Campus - Zanzibar and Pemba Branch for the September intake 2021. The application window for all programmes is open and will close on 14th August 2021 for Certificate and Diploma programmes whereas round one application for Degree programmes will close on 5th August 2021.

### APPLY NOW FOR THE FOLLOWING PROGRAMMES:

**CERTIFICATE PROGRAMMES**

| PROGRAMME | DURATION | ENTRY REQUIREMENT |
|---|---|---|
| i) Basic Technician Certificate in Youth Work | 1 year | The minimum entry qualification is four (4) passes at least D grade in any subject excluding religious subjects in a Certificate of Secondary Education Examination (CSEE). |
| ii) Basic Technician Certificate in Human Resources Management | | |
| iii) Basic Technician Certificate in Community Development | | |
| iv) Basic Technician Certificate in Library and Information Management | | |
| v) Basic Technician Certificate in Business Administration | | |
| vi) Basic Technician Certificate in Procurement and Supply | | |
| vii) Basic Technician Certificate in Information and Communication Technology | 1 year | The minimum entry qualification is four (4) passes at D grade in any subject excluding religious subjects in a Certificate of Secondary Education Examination (SCEE).The four passes must include a pass in Basic Mathematics and English Language. |
| viii) Basic Technician Certificate in Records, Archives and Information Management | | |
| ix) Basic Technician Certificate in Economic Development | | |
| x) Basic Technician Certificate in Accountancy | | The minimum entry qualification is four (4) passes at D grade in any subject excluding religious subjects in a Certificate of Secondary Education Examination (SCEE). The four passes must include a pass in Basic Mathematics. |

**DIPLOMA PROGRAMMES**

| PROGRAMME | DURATION | ENTRY REQUIREMENT |
|---|---|---|
| i) Ordinary Diploma in Social Studies | 2 years | Holders of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with at least four (04) relevant passes and Advanced Certificate of Secondary Education Examination (ACSEE) with at least one principle pass and one Subsidiary in any subject excluding the religious Subjects.<br><br>Holders of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with at least four (04) relevant passes (i.e. D grade or higher) including specific subject based on the course; and a relevant Basic Technician Certificate (NTA Level 4) recognized by NACTE or any other relevant one year certificate obtained from any learning institution registered by the Government or recognized by any Government body of the country of study. |
| ii) Ordinary Diploma in Human Resource Management | | |
| iii) Ordinary Diploma in Gender Issues and Development | | |
| iv) Ordinary Diploma in Library and Information Management | | |
| v) Ordinary Diploma in Community Development. | | |
| vi) Ordinary Diploma in Records, Archives and Information Management | | |
| vii) Ordinary Diploma in Economic Development | 2 years | Holders of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with at least four (04) relevant passes and Advanced Certificate of Secondary Education Examination (ACSEE) with at least one principle pass and one Subsidiary in any of the following subjects Economics, Commerce, Accounts, Physics, Chemistry, Biology, Pure Mathematics, Basic Applied Mathematics, Geography and other relevant subjects as per course specifications.<br><br>Holders of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with at least four (04) relevant passes (i.e. D grade or higher) including specific subject based on the course; and a relevant Basic Technician Certificate (NTA Level 4) recognized by NACTE or any other relevant one year certificate obtained from any learning institution registered by the Government or recognized by any Government body of the country of study. |
| viii) Ordinary Diploma in Accountancy | | |
| ix) Ordinary Diploma in Business Administration | | |
| x) Ordinary Diploma in Procurement and Supply | | |
| xi) Ordinary Diploma in Information and Communication Technology | 2 years | Holders of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with at least four (04) relevant passes and Advanced Certificate of Secondary Education Examination (ACSEE) with at least one principle pass and one Subsidiary in any of the following subjects Economics, Commerce, Accounts, Physics, Chemistry, Biology, Pure Mathematics, Basic Applied Mathematics, Geography, Computer and other relevant subjects as per course specifications.<br><br>Holders of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with at least four (04) relevant passes (i.e. D grade or higher) including specific subject based on the course; and a relevant Basic Technician Certificate (NTA Level 4) recognized by NACTE or any other relevant one year certificate obtained from any learning institution registered by the Government or recognized by any Government body of the country of study. |

**DEGREE PROGRAMMES**

| PROGRAMME | DURATION | ENTRY REQUIREMENT |
|---|---|---|
| i) Bachelor Degree in Management of Social Development | 3 Years | Form VI with at least two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from two subjects in History, Geography, English, Kiswahili, Biology, Chemistry, Agriculture, Commerce and any other Form six subject except religious studies.<br><br>Diploma in Social Studies **OR** Diploma in Gender and Development, Community Development/ Full Technician Certificate in Human Resource Management, Record Man agent, Social Work, Journalism, International Relational and Diplomacy, Secretarial Studies and Office Management Administration, Performing Arts with an average GPA 3.0 and above or 4 passes at 'O' Level (SCEE). |
| 1 Bachelor Degree in Economics of Development | 3 Years | Form VI with at least two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from two subjects: Economics, Accountancy, Commerce, Mathematics, Geography, Physics, Chemistry, Biology or Agriculture,<br><br>Diploma in Economic of Development **OR** Diploma in Community Development/ Full Technician Certificate in Procurement and Supply Management, Marketing, Accountancy, Financial Administration, Business Administration, Local Government Accountancy and Finance, Public Sector Finance, Management, with an average of GPA 3.0 and above or 4 passes at 'O' Level (SCEE). |
| 2 Bachelor Degree of Education in Geography and History | 3 Years | Form VI with at least two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from two subjects Geography and History subjects,<br><br>Diploma of Education in Geography and History with an average of C, Education Management and Administration, Adult and Continuing Education, with an average of GPA 3.0 and above or 4 passes at 'O' Level (SCEE). |
| 3 Bachelor Degree of Education in Kiswahili and English Languages | 3 Years | Form VI with at least two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from two subjects Kiswahili and English subjects,<br><br>Diploma of Education in Kiswahili and English with an average of C, Education Management and Administration, Adult and continuing Education, with an average of GPA 3.0 and above or 4 Passes at 'O' Level (SCEE). |
| 4 Bachelor Degree in Gender and Development | 3 Years | Form VI with at least two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from two subjects: History Geography, English, Kiswahili, Biology, Chemistry, Agriculture Commerce and any other Form six subject except religious studies.<br><br>Diploma in Gender and Development **OR** Diploma in Community Development/Full Technician Certificate, Nursing, Travel and Tourism, Police Sciences, Social Studies, Social Work, Economic of Development, Record Management, Human Resource Management with an average of GPA 3.0 and above **or** 4 passes at 'O' Level. |

216374802

# LHRC yabainisha mianya ukwepaji kodi

**Na Thobias Mwanakatwe**

TANZANIA inapoteza Dola za Kimarekani 299,485, 211 katika makusanyo ya kodi kila mwaka kutokana na mianya ya ukwepaji wa ulipaji kodi.

Aidha, wafanyakazi 700,000 wanafariki dunia kila mwaka duniani kutokana na kufanya kazi muda mrefu kama ilivyoainishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Hayo yalibainishwa juzi na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), wakati wa uzinduzi wa ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara nchini ya mwaka 2020/2021.

Ofisa Mwandamizi Kitendo cha Utafiti LHRC, Fundikila Wazambi, akiwasilisha ripoti hiyo, alisema kutokana na hali hiyo, Tanzania imetajwa kuwa miongoni mwa nchi 70 ambazo zinaongoza kwa kuwa na mianya ya ukwepaji kodi.

Alisema kati ya fedha hizo, kiasi cha Dola za Kimarekani 279,081,381 sawa na asilimia 93 ya fedha zinazopotea kwa sababu ya ukwepaji kodi unaofanywa na kampuni kwa kuhifadhi fedha za faida katika akaunti za nje.

Wazambi alisema kiasi hicho cha fedha ambacho Tanzania inapoteza katika mapato hayo kila mwaka kinaweza kulipa mishahara ya wauguzi (manesi) 135,577 mwaka mzima.

"Ripoti nyingine kuhusu kodi iliyotolewa na Mtandao wa Haki ya Kodi barani Afrika (TJNA) mwaka 2021 (CTHI 2021) inaonyesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi 70 duniani ambazo mifumo yake ya fedha na kodi inaweka mianya kwa kampuni za kimataifa kulipa kodi ya kampuni chini ya kiwango," alisema.

Kuhusu saa za kufanya kazi kwa wafanyakazi, alisema kumekuwa na changamoto ya waajiri kutozingatia kiwango cha saa za kufanya kazi ambapo asilimia 85 ya wafanyakazi walioshiriki katika utafiti walisema wapo huru kuondoka kazini baada ya saa za kawaida ya kufaya kazi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema utafiti wa ripoti hiyo ulilenga kuangalia ni namna gani biashara inaheshimu vipi haki za binadamu ambapo mikoa 15 ilifanyiwa utafiti kwa kupita katika taasisi za udhibiti, kampuni, wafanyakazi, madereva na wageni.

Henga alisema katika utafiti huo mambo makubwa waliyoyabaini ni suala la mikataba ya ajira ambayo imeshuka kwamba asilimia 59 ya wafanyakazi wengi walioshiriki walisema wana mikataba ya ajira kiwago ambacho kimeshuka ukilinganisha na mwaka jana.

"Idadi ya wafanyakazi wenye mikataba ya ajira ni pungufu kwa asilimia 25 ukilinganisha na idadi ya wafanyakazi wenye mikataba hiyo katika utafiti uliopita wa mwaka 2019 ambapo asilimia 84 walidai kuwa na mikataba ya ajira," alisema.

Alisema utafiti huo pia umebaini obwe la kukosekana kwa uelewa juu ya sheria za kazi za ajira kwa wafanyakazi, ambapo mkoa wa Tabora ndio ulioongoza kwa kuwa na asilimia kubwa zaidi ya wafanyakazi wasio na uelewa wa kutosha kuhusu sheria na kanuni za kazi.

Henga alitoa wito kwa serikali kutembea katika kampuni na taasisi kujionea hali halisi ilivyo badala ya kusubiri kuletewa taarifa ambazo nyingi zinakuwa za kupikwa.

# CCM: Tanzania sasa hakuna mapambano ya demokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema Tanzania hakuna mapambano ya demokrasia kwa kuwa mageuzi na mabadiliko toka chama kimoja na kuingia vyama vingi yamefanyika kwa ridhaa na kwa mujibu wa sheria.

Kauli hiyo imetolewa jana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu.

Kiongozi huyo alikuwa akitoa ufafanuzi kuhusu kauli iliyotolewa na Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, kuwa Tanzania iko katika mapambano ya demokrasia baada ya kutoa madai ya kutekwa kwa Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe.

Shaka alisema masuala ya ndani ya nchi kwa mujibu wa sheria hufanyika pale inapobidi na mamlaka za utawala hazihitaji kibali toka jumuiya zozote za nje au za ndani.

Alisema jumuiya za kimataifa zikiwamo taasisi zinazoshughulikia haki za binadamu, demokrasia na utawala bora, zina taratibu na mipaka zinapotaka kujua yanayoendelea au kujiri katika taifa fulani na hazina haki ya kuziamuru mamlaka zilizopo kufuata matakwa yao.

"Polisi wamethibitisha kumkamata Mbowe na wala hajatekwa kama Mnyika na CHADEMA wanavyodai. Matamshi yao yamelenga kujenga chuki na kuchafua taswira ya nchi yetu kwenye Jumuiya ya Kimataifa. Tanzania ni nchi huru inayoongozwa kwa misingi ya utawala wa sheria," alisema Shaka.

Shaka alisema demokrasia ipo kisheria na kikatiba zaidi na Tanzania ni nchi ya kupigiwa mfano katika kuzingatia ustawi wa haki za binadamu na maendeleo ya demokrasia.

"Kutumia kivuli cha demokrasia kuvunja sheria huko ni kuinajisi demokrasia. Vyama vyote vya siasa vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria hivyo vina wajibu wa lazima kuwa mfano kwa kutii na kutekeleza sheria za nchi," alisema na kuongeza.

"Katika hili niwakumbushe CHADEMA moja ya misingi muhimu ya demokrasia ya kweli ni pamoja na kuheshimu na kutekeleza kwa usawa utawala wa sheria. Ikiwa wanaaishi demokrasia na wanaitaka ionekane ikiishi ni vyema wakaheshimu utawala wa sheria ambao hakuna mtu yupo juu ya sheria."

Alisema kukamatwa kwa kiongozi yeyote awe wa chama tawala au wa upinzani, si shambulio dhidi ya demokrasia kama inavyodaiwa na CHADEMA.

"Mnataka demokrasia, utawala wa sheria na haki, halafu muda huo huo mnamtaka Rais aingilie mahakama akiuke Katiba na sheria za nchi kwa maslahi yenu hili halikubaliki kabisa. Serikali ya Rais Samia itasimamia Katiba, sheria, haki na usawa wakati wote," alisisitiza Shaka.


| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Bachelor Degree in Human Resources Management | 3 Years | · Form VI with at least two Principal Passes at D grade with a total of 4.0 points from the following subjects; English, History, Kiswahili, geography, Agriculture, Economics and Commerce.<br>· Diploma in Human resource Management **OR** Diploma in Gender and Development, Community Development/ Full Technician Certificate, Social Studies , Record Management, Social Work, Journalism, International Relation and Diplomacy, Secretarial Studies and Office Management with an average of GPA 3.0 and above **or** 4 passes at 'O' Level (SCEE). |
| 6 | Bachelor Degree of Education in Geography and Kiswahili | 3 Years | · Form VI with at least two Principal passes at D Grade with a total of 4.0 points from Geography and Kiswahili subjects,<br>· Diploma of Education in Kiswahili and English Geography and Kiswahili with an average of C, Education Management and Administration, Adult and continuing Education, with an average of GPA 3.0 and above or 4 Passes at 'O' Level (SCEE). |
| 7 | Bachelor Degree of Education in Geography and English | 3 Years | · Form VI with at least two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from Geography and English subjects.<br>· Diploma of Education in Geography and English with an average of C, Education Management and Administration, Adult and Continuing Education, with an average of GPA 3.0 and above or 4 passes at 'O' Level (SCEE). |
| 8 | Bachelor Degree of Education in History and English | 3 Years | · Form VI with two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from History and English subjects<br>· Diploma of Education in History and English with an average of C, Education Management and Administration, Adult and Continuing Education, with an average of GPA 3.0 and above or 4 passes at 'O' Level (SCEE). |
| 9 | Bachelor Degree of Education in History and Kiswahili | 3 Years | · Form VI with two Principal passes at D grade with a total of 4.0 points from History and Kiswahili subjects.<br>· Diploma of Education in History and Kiswahili with an average of C, Education Management and Administration, Adult and Continuing Education, with an average of GPA 3.0 and above or 4 passes at 'O' Level (SCEE) |

**MASTER'S PROGRAMMES**

| PROGRAMME | DURATION | ENTRY REQUIREMENT |
|---|---|---|
| Master in Human Resource Management. | 2 Years | · A candidate must hold at least a second class bachelor's degree or advanced diploma in any field(s) of study from recognized institutions of higher learning.<br>· A candidate with PASS Degree/Advanced diploma will also be considered by the academy upon producing evidence of having obtained an examined postgraduate or professional qualification from approved bodies<br>· A candidate who holds unclassified degrees should have an average credit of B or above. A candidate holding a degree or advanced diploma from foreign institutions should be certified by the Tanzania Commission for Universities (TCU) before being considered for admission. |

**MODE OF APPLICATION**

1. All applications must be through the Online Admission System (OSIM) of the Mwalimu Nyerere Memorial Academy (MNMA) available in our website: www.mnma.ac.tz or visit the Admission Office at the MNMA – Kivukoni Campus in Dar es Salaam, Karume Campus and Pemba Branch in Zanzibar for more assistance.
2. Each applicant for Certificate, Diploma and Bachelor Degree Programmes is required to pay an application fee of TShs. 10,000/= for Tanzanian Citizens and US$ 10 for Non-Tanzanian Citizens. Master Degree applicants shall pay application fee of TShs. 50,000 for Tanzanian Citizens and US$ 50 for Non-Tanzanian Citizens.

**NOTE:** All payments should be through Government Electronic Payment Gateway (GePG) which can be found on OSIM from the Academy's website.

**For more information please contact:**

**Rector**
The Mwalimu Nyerere Memorial Academy,
P.O. Box 9193,
**Dar es Salaam**

Fax No: (022) 2820816
Email: rector@mnma.ac.tz or admission@mnma.ac.tz
Website: www.mnma.ac.tz

**OR Call the Following Numbers:**

Kivukoni Campus: (022) 2820041/ 2820047/ 0712176450 0655460062 0714472751 0787531043 0623396549

Karume Campus: (024)2250315 0713684663

Pemba Branch: (024)2452200 0655108108 0763988177

216374802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili wa wachezaji waachiwe makocha

**HIVI** sasa klabu zote za Ligi Kuu Tanzania Bara, ligi daraja la kwanza zipo kwenye haraka za kusajili wachezaji wapya ili kuimarisha vikosi tayari kwa msimu ujao.

Ligi ambayo ilimalizika mwezi uliopita kwa Simba kutwaa ubingwa kwa mara ya nne mfululizo, sasa inazipa nafasi za klabu kujipanga kwa ajili ya msimu mpya.

Timu nne zitawakilisha nchi kwenye mashindano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, hivyo usajili wa wachezaji muhimu zaidi kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao. Na sasa timu zimeingia kwenye vita ya usajili ingawa tayari kuna nyingine zilishaanza kusajili mapema tu na hii ni kutokana na ligi ya msimu huu kuchelewa kuisha sababu ya janga la Corona.

Tumeshaanza kuona viongozi wa timu kadhaa hapa nchini wakisafiri kwenda nje ya nchi kufuatilia wachezaji na shughuli nyingine za kitimu. Wakati timu zinaenda kwenye vita ya usajili zinapaswa kukumbushwa kuwa, zinatakiwa kusajili kulingana na upungufu na siyo kusajili kwa sifa kisa zimeona timu zingine zinafanya hivyo.

Msimu uliopita tulishuhudia sajili nyingi sana na wachezaji baadhi walikuwa wakipokelewa kwa makundi makubwa ya mashabiki wa timu husika hivyo basi, Nipashe tunaona viongozi wayaachie kazi mabenchi ya ufundi yafanye kazi yao na wao wabaki kwenye suala la kutoa fedha ili kukamilisha usajili.

Makocha wanatakiwa wasiingiliwe linapokuja suala la kiufundi, maana ndiyo kazi waliyosomea na viongozi wadili na suala la kiutawala na kuingilia majukumu yasiyomuhusu.

Kocha anatakiwa kuachwa afanye usajili wa wachezaji anaowataka na hata ikitokea wakashindwa kufanya vizuri basi anapotimuliwa kazi, basi iwe kwa haki, kwamba kwa kuwa mlimpa kila alichokihitaji na yeye akashindwa kuwapa furaha, basi hakuna budi kumwondoa, hapo hamna dhambi kabisa maana kila upande umetenda haki.

Viongozi msisajili wachezaji ambao mwisho wa siku wanaishia kukaa benchi au jukwaani.

Tumeona wachezaji wakali wakitoka huko timu za kawaida wanaenda timu kubwa wakiwa na viwango vya juu, lakini huko wanakutana na wakubwa zaidi yao na kujikuta akiishia benchi na kuua vipaji vyao.

Au kiongozi utaona anasajili tu mchezaji ilimradi anajua anapata asilimia kumi wao huita 'ten percent' sasa hii inakuwa inaharibu soka, sawa inawezekana wakati mwingine kamali inakubali kwa mchezaji kuwika kwa kuwa msaada lakini mara nyingi huwa wanafeli. Tunajua kwamba, sasa hivi wachezaji wengi wanaangalia fedha, lakini ni bora ukakaa sehemu ambayo unafanya kazi yako kwa amani bila presha na unalipwa kama kawaida hata kama ni fedha ya kawaida kuliko kwenda sehemu ambayo unalipwa sana, huchezi hata benchi hukai unaishia jukwaani, hapa unaua kipaji.

Ili soko liweze kuonekana inatakiwa uonekane unacheza sasa kama umekubali kulipwa fedha nyingi na unaenda kuishia kukaa jukwaani ni kazi bure.

Makocha nao msikubali tu kupelekwa na viongozi wakati mkijia fika kuwa nyinyi ndio wataalamu wa benchi la ufundi na mnajua wachezaji gani wanaofaa kwenye kikosi chako.


Kazi ya kocha ni kupendekeza majina ya wachezaji anaowahitaji na ambao anaona wanaweza kuwa msaada kwa timu, na hivyo mkiwaachia viongozi wawasajilie wachezaji, mzigo baadaye unaangukia kwenu.

Hivyo basi, Nipashe tunaona kwamba, makocha wasiingiliwe kwenye kazi ya usajili ili waweze kupata nyota wazuri ambao wataweza kuisaidia timu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni wakati wa TFF kuleta waamuzi nje

Na Adam Fungamwango

**NI** ukweli usiopingika kuwa soka la Tanzania kwa sasa limepiga hatua kubwa. Ingawa badio kuna matatizo kadhaa ikiwemo baadhi ya timu kutokuwa sawa kiuchumi, lakini soka la Tanzania limeanza kuvutia nchi nyingi na kuanza kulifuatilia.

Hii inatokana na sababu mbalimbali ikiwemo mechi nyingi kuonyeshwa kwenye televisheni. Ligi ya Tanzania ni moja kati ya ligi ambazo mechi zake nyingi zinaonyeshwa kwenye televisheni, tofauti na nyingi kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na kati ambapo ni baadhi tu ya mechi zinazoonyeshwa.

Hapa nchini hata Mbeya City ikicheza na Mwadui mechi inakuwa laivu.

Sababu nyingine ni uwezo na wachezaji wengi wa kigeni, na hasa kutoka kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kama vile Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi, Rwanda, Zambia, Zimbabwe, Uganda, Kenya, na nchi zingine kama Ghana, Ivory Coast na nyingine.

Kuwepo kwa baadhi ya wachezaji wa nchi hizo kunasababisha wananchi wengi wa nchi hizo kufuatilia maendeleo ya wachezaji wao, hivyo kuvutiwa na soka la Tanzania.

Tuliona kwenye Mei 8 mwaka huu, ilipopangwa kuchezwa mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga na kushindwa kufanyika, baadhi ya mashabiki wa soka walitoka nje ya nchi.

Tuliona tawi la SImba kutoka Kitwe nchini Zambia. Hawa walikuja kuwaunga mkono wachezaji wa timu hiyo ambao ni Wazambia wenzao, Clatous Chama na Rally Bwalya.

Tangu timu ya Simba iingie hatua ya Robo Fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2019, Ligi ya Tanzania imekuwa ikiangaliwa kwa jicho la tatu na mashabiki wa wengi Afrika.

Mwaka huu pia Simba imefanikiwa pia kutinga hatua hiyo. Wakati Ligi ya Tanzania ikizidi kutingisha kwa ubora, pamoja na soka la Bongo kwa ujumla, lakini kuna baadhi ya matatizo yanabidi yarekebishwe ikiwemo uchezeshaji.

Baadhi ya waamuzi wameonekana kuchezesha kwa woga, hasa mechi zinazozihusu timu kubwa kama Simba na Yanga.

Mechi zote tatu, ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu na wa pili, pamoja na fainali ya Kombe la FA, waamuzi walionekana kuchezesha kwa wasiwasi na kufumbia baadhi ya matukio ambao wanayaona na yapo karibu kabisa.

Waamuzi wanashinda kutolea maamuzi rafu mbaya ambazo si za kimpira, bali ni za kutaka kuvunjana na kuhatarishiana amani.

Wanafanya hivyo kwa wasiwasi. Labda kwa sababu wameshaanza kuonyeshewa vidole. Ikumbukwe hata kabla ya mechi ta fainali ya FA, Yanga iliandika barua ya kutokuwa na imani na mwamuzi Ahmed Aragija. Kwa kiasi fulani hii ilimfanya akose kujiamini, hasa kipindi cha kwanza.

Inawezekana kabisa Yanga ndiyo walikuwa wanakihitaji. Kumpa presha mwamuzi.

Kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano ya Kombe la FA, Shirikisho la Soka Nchini pamoja na Bodi ya Ligi inabidi kubadilisha kanuni ili kuruhusu kuleta waamuzi kutoka nje kwenye baadhi ya mechi, ikizekana.

TFF na Bodi ya Ligi ambayo naona mara nyingi inalaumiwa sana na mashabiki kwa makosa ambayo wakati mwingine siyo yao, inaweza kuepuka hili kwa kuweka kanuni hii, ili baadhi ya mechi za Simba na Yanga, Simba dhidi ya Azam, au Yanga dhidi ya Azam kuchezeshwa na waamuzi kutoka nje ya nchi kama inavyokuwa kwa baadhi ya nchi za wenzetu.

Kwa hali iliyofika sasa ambapo soka la Tanzania wakati mwingine linachezwa kisiasa sana tena nje ya uwanja, kabla ya uwanjani kwenyewe kwa kuwapa presha na kuwatisha waamuzi, ni wakati wa kubadilika kabla hali haijawa mbaya kwa TFF na Bodi ya Ligi.

Siyo kama waamuzi wa Tanzania hawajui, ila ni kuondoa lawama zisizo la msingi kutoka kwa mashabiki na viongozi wa timu hizi.

Kwanza kabisa waamuzi walitoka nje, wanakuwa hawana presha au homa ya Simba na Yanga kama wanavyopata waamuzi wa Bongo.

Watakapochezesha hata kama ni dakika ya kwanza ikipatikana penalti, atatoa kwa sababu hata hofu yoyote. Kama ni kadi nyekundu basi itatoka. Yoyote anayecheza mpira vurugu basi mwamuzi atamuonya kwa vile inavyopaswa. Na mechi ikiisha wanaondoka nchini kwao. Hii kwanza itapunguza lawama si kwa viongozi wa soka, bali hata kwa waamuzi wetu hasa wanapochezesha mechi hizi kubwa.

Niwakumbushe tu kuwa mashabiki wa Simba na Yanga wanakuwa na imani zaidi na waamuzi kutoka nje kuliko wa ndani. Na hata akifanya kosa lolote la kibinadamu, wataamini kuwa ni bahati mbaya, tofauti na atakavyofanya mwamuzi wa Kitanzania. Watasema amehongwa.

Nasema hili kwa kujenga, kuwaodoa TFF na Bodi ya Ligi pamoja na waamuzi wetu kwenye lawama zisizo na msingi ili Ligi yetu izidi kukua na kuheshimika.

Kote ambako ligi zao zinaheshimika Afrika, 'dabi' zao zinachezeshwa na waamuzi kutoka nje.

Anakuja mwamuzi, anachezesha, timu mmoja inafungwa hakuna wa kumtupia lawama kwa sababu mwamuzi ni mgeni, wanaoshangilia wanashangilia na waliofungwa wanakwenda kulala.

Natumai hii inaweza kuanza msimu ujao.

HABARI KITAIFA

# Waziri ataka mikopo wahitimu wa ufundi

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amewataka viongozi wa mikoa na halmashauri kutoa kipaumbele cha mikopo kwa wahitimu wa ufundi stadi ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiri wengine.

Waziri Mhagama aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua shughuli za utekelezaji wa programu ya mafunzo ya uanagenzi inayofadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu katika Chuo cha VETA Busokelo, Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya.

"Nawaomba sana viongozi wa mikoa na halmashauri mtoe kipaumbele cha mikopo kwa hawa vijana ili wapate mitaji na vifaa vya kufanyia kazi baada ya kuhitimu. Tena ukiwapa hawa watachangia kuongeza mapato kwenye halmashauri yako na unakuwa na uhakika wa mikopo yako kurejeshwa, maana tayari wana ujuzi," amesema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Dk. Pancras Bujulu, alishukuru serikali kwa kuendelea kuwezesha vijana kupata mafunzo ya ufundi stadi na aliahidi kuwa mamlaka hiyo itahakikisha vijana hao wanapata mafunzo bora yatakayowawezesha kujiajiri baada ya kuhitimu.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa programu hiyo katika Chuo cha VETA Busokelo, Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Wilbert Bendera, alisema jumla ya vijana 173 wa Halmashauri hiyo ya Busokelo walipata fursa ya mafunzo hayo katika fani za Useremala, Ushonaji, Umeme, Matumizi na Ukarabati wa Kompyuta na Utengenezaji Vifaa vya Kielektroniki, ingawa hadi sasa walioripoti ni 127 tu, sawa na asilimia 74.

Kufuatia taarifa hiyo, Waziri Mhagama aliuagiza uongozi wa chuo hicho kushirikiana kwa karibu na Mbunge wa Jimbo la Busokelo, uongozi wa Halmashauri ya Busokelo, pamoja na Diwani wa Kata ya Lufilyo kuhakikisha nafasi za vijana ambao hawakuripoti zinajazwa mara ili wananchi wa eneo hilo wanufaike na fursa hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James (wapili kulia) akikabidhi cheti kwa mwanafunzi wa darasa la saba Shule ya St Anne Marie ya Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam, Shigongo Ndaki, aliyefanya vizuri somo la stadi za kazi kwenye mahafali ya 18 yaliyofanyika mwisho mwa wiki shuleni hapo. Kulia ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Jasson Rweikiza na kushoto ni Mkuu wa Shule, Gladius Ndyetabura. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Watalii 550 kutoka Israel kutua nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATALII 550 kutoka Israel wanatarajiwa kuwasili nchini kwa makundi tofauti kwa ajili ya kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Paschal Shelutete, watalii hao watatembelea hifadhi za taifa zilizoko Kaskazini mwa Tanzania pamoja na eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Shelutete alisema: "Kundi la kwanza la watalii 150 litawasili leo kwa ndege binafsi kutoka nchini Israel katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) majira ya saa 11 alfajiri."

Alisema kundi la pili la watalii litawasili Agosti 9, mwaka huu likiwa na watalii 200 na kundi la tatu litawasili Agosti 16, mwaka huu na watalii wote hao watashukia Uwanja wa Ndege wa KIA.

Shelutete alisema ujio wa watalii hawa kutoka Israel unatokana na juhudi kubwa za utangazaji wa utalii katika soko linalokuwa kwa kasi nchini humo.

Alitaja sababu nyingine iliyoongeza idadi hiyo ya watalii ni pamoja na jitihada zilizochukuliwa na serikali ya awamu ya sita katika kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona.

"Ongezeko hili pia kinatoka na kuzingatia kanuni na mwongozo inayotolewa na Shirikaa la Afya Duniani (WHO), ikiwamo utolewaji wa chanjo ya ugonjwa wa virusi vya corona," alisema Shelutete.

Aidha, alitaja sababu nyingine ni pamoja na serikali kufungua ubalozi katika nchi ya Israel, hali ambayo imeleta hamasa kubwa kwa wananchi hao kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na ubalozi huo.

Vilevile, Shelutete alisema watalii hao wataendelea kuja nchini, kwamba makundi mengine makubwa yanatarajiwa kuwasili nchini Septemba na Oktoba, mwaka huu.

Alisema kwa kipindi cha mwaka jana Tanzania ilipokea idadi kubwa ya watalii zaidi ya 1,000 kutoka Israel, ambao walipata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali hapa nchini.

Aliongeza kuwa watalii hao wanatarajiwa kupokelewa na viongozi mbalimbali wa kiserikali sambamba na hafla fupi itakayofanyika uwanjani hapo.

# CRDB ilivyoongeza faida kabla ya kodi

**Na Christina Mwakangale**

BENKI ya CRDB imeongeza faida kabla ya kodi na kufikia Sh. bilioni 127 ikilinganishwa na Sh. bilioni 100 iliyorekodiwa katika kipindi hicho mwaka jana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, aliyasema hayo katika taarifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam.

Alisema benki hiyo inaendelea kudumisha utendaji kazi mzuri wa kifedha baada ya kutangaza ongezeko la asilimia 26.6 katika taarifa ya fedha ya nusu ya kwanza kwa mwaka 2021.

"Faida Kabla ya Kodi imeongezeka kufikia hadi Shilingi bilioni 127 kulinganisha na shilingi bilioni 100 iliyorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2020.

"Amana, mikopo na jumla ya mali, imeendelea kukua. Jumla ya mali imeongezeka kwa asilimia 15.2 kutoka shilingi trilioni 7.0 hadi trilioni 8.1, Amana imeongezeka kwa asilimia 10.6 kutoka Sh. trilioni 5.5 hadi Sh. trilioni 6.1," alisema Nsekela.

Alisema kwa upande wa jumla ya mikopo iliyotolewa imeongezeka kwa asilimia 15.7 kutoka Sh. trilioni 3.6 mwaka jana hadi Sh. trilioni 4.2, mwaka huu.

Kadhalika, alisema faida ya benki hiyo pia imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kushuka kwa uwiano wa mikopo chechefu hadi asilimia 4.4 kutoka 4.8 mwaka jana, ikionyesha usimamizi bora wa mikopo.

"Tumeshuhudia utendaji mzuri nusu ya kwanza ya mwaka 2021. Faida baada ya kodi imeongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 89, faida kubwa kulinganisha hata kabla ya corona. Tunaendelea kusonga mbele kwa kasi katika baadhi ya maeneo muhimu ya mkakati wetu wa biashara.

The Guardian Limited

VACANCY

Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

NOTE: This is a commission Based Position

Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.

216387602

# Tanzania yatafuta soko la maparachichi Afrika Kusini

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI imesema inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Afrika Kusini kwa ajili ya kupata soko la maparachichi yanayolimwa katika maeneo mbalimbali nchini ili kutatua kero ya wananchi kuingia hasara kwa matunda hayo kutupwa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Rungwe baada ya kutembelea mashamba ya kiwanda cha maparachichi cha Kampuni ya Kuza Afrika Ltd kilichopo katika Kijiji cha Ilolo, Kata ya Kiwira.

Kiwanda hicho ni miongoni mwa wanunuzi wakubwa wa maparachichi yanayozalishwa na wananchi wa Wilaya ya Rungwe na kimekuwa kikinunua yaliyoharibika kwa ajili ya kuzalishia mafuta ya kupaka na bidhaa zingine.

Vilevile, Waziri Mkuu alisema mwekezaji wa kiwanda hicho ndiye aliyegundua soko la maparachichi hayo Afrika Kusini na akaanza mchakato wa kuanza kupeleka matunda hayo na serikali imeamua kuungana naye kutafuta soko hilo. Aliwataka wananchi wa Wilaya ya Rungwe pamoja na maeneo mengine ambayo zao hilo linastawi kuendelea kuzalisha kwa wingi kuwa soko hilo ni la uhakika na litapatikana kwa namna yoyote ili wakulima wapate faida zaidi.

"Wizara ya Kilimo imepewa kazi ya kusimamia kilimo cha maparachichi ikiwa ni pamoja na kuwatafutia wakulima mbegu bora, kutunza miche shambani pamoja na kutafuta masoko, hivyo nawaomba wakulima limeni kwa nguvu," alisema Majaliwa na kuongeza.

"Nawaagiza maofisa kilimo kuanzia wa mkoa mpaka wilaya kuhakikisha wanawasaidia wakulima kulima kisasa zao hili, wakurugenzi waondoeni maofisa kilimo halmashauri wakafanye kazi kwa wakulima, waanzishe mashamba darasa ya kuwafundishia wakulima," alisema.

Alimpongeza mwekezaji wa Kiwanda cha Kuza Afrika kwa kuwasaidia wakulima kupata soko la mazao yao pamoja na kutunza vizuri shamba lake lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 300.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema Wilaya ya Rungwe ni miongoni mwa zinazozalisha maparachichi kwa wingi, lakini tatizo ni upatikanaji wa soko la uhakika.

Alisema Kiwanda cha Kuza Afrika ndio moja ya suluhisho la awali ya tatizo hilo kutokana na kuanza kununua mazao ya wakulima na suluhisho la kudumu ni kupata soko la Afrika Kusini ambalo ni la uhakika. Alisema kwa sasa wizara pamoja na Menejimenti ya Kiwanda cha Kuza Afrika wanaendelea kufuatilia taratibu za kupata soko hilo na kwamba mpaka sasa wapo kwenye hatua za mwisho za kupata soko hilo.

"Tutahakikisha tunasimamia kwa umakini kilimo cha zao hili ambalo kwa sasa ni miongoni mwa mazao yenye soko kubwa duniani, sasa sisi kama wizara lazima tuhakikishe tija inaongezeka," alisema Bashe.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alisema ili kuhakikisha wakulima wanapata tija, serikali imeanza mkakati wa kuboresha miundombinu ya barabara zinazopita mashambani ili kurahisisha usafirishaji.

Alisema kwa sasa serikali imeshatoa Sh. bilioni moja katika kila jimbo nchini kwa ajili ya kuboresha barabara ambazo zinasimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Waziri Mkuu Majaliwa alianza jana ziara yake ya siku sita mkoani Mbeya ambapo mbali na kiwanda hicho pia alizindua Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) cha Wilaya ya Busokelo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Sophia Jongo, akitoa taarifa ya hali ya ulinzi na usalama ya mkoa huo kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo (kushoto), wakati wa ziara ya kikazi iliyofanyika leo mkoani Tabora. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Madiwani waikataa kampuni kupewa zabuni

**Na Said Hamdani,** LINDI

KIKAO cha Baraza la Madiwani, Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, mkoani hapa kimeikataa Kampuni ya Mafubilo General Supplies Ltd., kupewa zabuni ya kuendesha maghala kwa madai ya kukosa sifa ikiwamo madai ya kujihusisha na wizi wa mazao ya wakulima.

Uamuzi huo ulitolewa na madiwani hao kwenye kikao kilichofanyika Nachingwea.

Walisema hawako tayari kuipatia zabuni ya uendeshaji maghala kampuni hiyo kwa madai ya kukosa sifa kama sheria ya zabuni inavyoelekeza.

Veronica Mkotha, Diwani wa Viti Maalum ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Omari Mbinga, Ally Chitanda na George Kambona, walidai msimu 2019/2020 kampuni hiyo iliwaibia wakulima tani 35 za korosho zenye thamani ya Sh. 73,666,484.

Walisema kwa kitendo hicho kampuni hiyo imeondolewa sifa ya uendeshaji maghala kama sheria inavyoelekeza, huku wakisisitiza sheria ifuatwe kwa kampuni iliyoshika nafasi ya pili wakati wa kinyang'anyiro cha uombaji zabuni ipewe kuendesha maghala.

Madiwani hao walidai pia kitendo cha kamati iliyohusika na mchakato wa kumpata mzabuni kuipitisha tena kampuni hiyo ni ukiukwaji wa sheria kwa kuwa tayari Mafubilo inakabiliwa na kesi mahakamani kutokana na upotevu wa korosho za wakulima.

"Sheria ya zabuni ipo wazi mzabuni mwenye matatizo haruhusiwi kupewa kazi ya uendeshaji maghala, Mafubilo tayari ina kesi mahakamani inapewaje tena zabuni hii?" Walihoji madiwani hao. Pia, wameonyesha kushangazwa na wataalamu wa halmashauri yao (Nachingwea), hasa kamati iliyohusika kusimamia mchakato wa kupitia majina ya waombaji, kuipitisha tena kampuni hiyo, huku ikielewa kampuni hiyo imepoteza sifa kwa mujibu wa sheria.

Kampuni ya Mabufilo iliyokuwa inaendesha ghala kuu la Pachani, Wilaya ya Nachingwea ilifikishwa mahakamani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi, ikituhumiwa kufanya udanganyifu wa kughushi nyaraka ya kupokea tani 35 za korosho kutoka kwa wakulima wawili na kujipatia Sh. 73,666,484.

# Tembo wazidi kuua, kujeruhi wanavijiji

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

KASI ya tembo kuua na kujeruhi wanavijiji katika maeneo kadhaa nchini imeendekea baada ya mtu moja kufa na wengine watatu kujeruhiwa na wanyama hao.

Hayo yamebainishwa na Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Limbega, Hassan Ally wakati akizungumza na Nipashe, na kwamba mbali na matukio hayo pia wanyama hao waliharibu zaidi ya hekari 600 za mashamba ya wakulima.

Limbega alisema tukio la kwanza lilitokea Julai 7, mwaka huu katika Kijiji cha Muhuwesi ambapo kijana wa amika 15, Lazack Shaibu Adam, alikufa baada ya kushambuliwa na tembo wakati akienda shambani kwa ajili ya kumjulisha mama yake juu ya uwapo wa makundi ya tembo katika eneo hilo.

Alisema baada ya tukio hilo Julai 23, Ofisi yake pia ilipokea taarifa za tukio la tembo kumjeruhi Emmanuel Hadrianob (35).

Alisema tukio hilo lilitokea katika Kijiji cha Kazamoyo Kata ya Lukumbule, na kwamba majeruhi alikimbizwa katika Hospitali ya Serikali ya Wilaya ya Tunduru kwa matibabu, na hali yake inaendelea vizuri.

Alisema Julai 26 ofisi yake ilipokea taarifa za tembo kumjeruhi Amasha Daniel Masoweni (35), mkazi wa Kijiji cha Ujenzi Mjini Tunduru wakati akienda kuchukua ng'ombe katika kambi ya wafugaji iliyopo katika kijiji Kajima.

Alisema chanzo cha wanyama hao kuzagaa katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo ni idadi kubwa ya mifugo kuchungiwa kwenye maeneo ya kingo za hifadhi hali, ambayo imekuwa ikiwafanya tembo kukimbia kelele za kengera zilizofungwa kwenye mifugo pamoja na harufu ya madawa ya kuogeshea mifugo hiyo.

Limbega alisema ofisi yake kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi kutoka ofisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na hifadhi za jamii wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kwenda kuwafukuza tembo na kuwerejesha kwenye maeneo ya malisho yao, ingawa juhudi zao zimekuwa zikigonga mwamba kutokana na wanyama hao kurudi tena maeneo ya vijijini.

## Ziara ya Mwambe yaleta nuru Masasi

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

ZIARA ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), ambaye ni Mbunge wa Masasi Mjini, mkoani Mtwara, Geoffrey Mwambe, amefanikisha kufanya maboresho kadhaa yenye kuleta kwa maendeleo jimboni humo.

Akizungumza baada ya kutembelea Kata ya Matawale na kukabidhi mabati 200 kwa ushirikiano na Benki ya Posta Tanzania (TPB) kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ya Gereza la Wilaya ya Masasi, Mwambe alisema serikali imedhamiria kuleta maendeleo na kutatua changamoto zinazowakabili na kuwataka wakazi hao kuwa na imani ya serikali yao.

"Ninakabidhi mabati haya kwa ushirikiano na wenzetu wa TPB, lakini nataka niwaambie kuwa serikali ipo pamoja nanyi na ina malengo mazuri kuhakikisha tunafikia maendeleo na kuondoa changamoto, hivyo niwaombe muwe na imani na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan."

Alisema serikali kwa kuona umuhimu wa afya kwa wakazi wa maeneo hayo, imeamua kuwapatia Sh. milioni 500 kwa ajili ya ukarabati mkubwa na upatikanaji wa dawa katika Hospitali ya Mkomaindo.

kwa upande wa elimu, Mwambe mbali ya kuchangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi darasa, alisema serikali imewapatia Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Shule Sekondari ya Matawale.

Aliongeza kuwa kwa kuona umuhimu wa miundombinu Rais Samia amewapatia Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuweka rami barabara za Masasi mjiji, huku pia milioni 700 zikitumika kwenye ukarabati njia zinazounganisha jimbo hilo na majimbo mengine.

Aidha, mbunge huyo aliwaomba wananchi hao kuwa wavumilivu kwenye suala la maji kwa kuwa amehakikishiwa na Idara ya Maji RUWASA kuwa ndani ya mwaka huu kitajengwa kisima kirefu kitakachowasaidia kupata maji ya kutosha na kupunguza kero ya maji.

Kwa upande wake Hamisi Mnela, Diwani wa Matawale, alimhakikishia Mwambe kuwa wananchi wako tayari kushirikiana naye kuhakikisha maendeleo yanafikiwa jimboni.

"Mimi nataka nikuhakikishie kuwa sisi tuko pamoja na wewe na tunatambua na kuthamini jitihada zako za kuleta maendeleo kwetu, hivyo na sisi hatutokuangusha na Mungu akusimamie kukamilisha mazuri uliyonayo kwetu," alisema Mnela.

# Kunenge awafunda watumishi wa afya

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema watumishi wa kada ya afya ni kati ya kundi ambalo linatakiwa kufanya kazi kwa nidhamu na kufuata maadili, kutokana na kushughulika zaidi na afya za watu.

Akiwa katika mahafali ya 54 ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi kilichopo Tumbi Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, alisema, hatarajii kusikia mtumishi kutoka katika chuo hicho anakuwa mmoja wa wanaokiuka maadili ya kazi, kwani itakuwa imemchafulia pia na yeye, ambaye alishiriki na kutoa vyeti kwa wahitimu hao.

Kunenge alisema nidhamu kazini na kufuata maadili ni jambo la muhimu wakati wa kutoa huduma kwa watu, ambapo kundi la kada ya afya linatakiwa kuzingatia hayo kuepusha matatizo kwa watu wanaowahudumia.

"Katika baadhi ya taaluma ambazo unatakiwa kuwa na nidhamu ya kazi ni hii ya afya, kwa sababu muda mwingi mnashughulika na maisha ya watu, sitegemei mkatangazike vibaya baada ya kutoka hapa mtakua mmenitangaza na mimi vibaya, inatarajia kupata sifa nzuri mkiwakilisha chuo na mgeni rasmif," alisema Kunenge.

Aidha, aliwataka wakufunzi wa chuo hicho kuhakikisha wanatoa elimu bora inayokidhi mahitaji ya wanachuo, kwa kufanya utafiti na watakapopata majibu yanayoipa shida jamii kuyafanyia kazi kwa wakati uliopo ili wahitimu wakashughulike na majibu ya utafiti.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Stephen Mdembwe, alisema kundi kubwa la vijana wanaoomba kujiunga na chuo hicho hukosa nafasi, kutokana na uwezo mdogo wa kupokea wanachuo.

"Chuo kimekuwa kikipata maombi zaidi ya 5,000 waombaji wenye sifa na kwa miundombinu iliyopo chuo kina uwezo wa kupokea wanachuo 160 kwa madarasa mawili yaliyopo, hali inayodhihirisha umuhimu wa kupanua chuo hiki ili kuongeza idadi ya wataalamu wa afya kutokana na ongezeko la mahitaji," alisema.

Mdembwe alisema kwa mujibu wa NACTE katika udahili uliokamilika kwa mwaka wa masomo 2020/2021, wahitimu wenye vigezo waliomba nafasi za masomo kwa kozi mbalimbali kati yao 3,354 pekee ndio waliopata nafasi katika vyuo vya serikali na 10,720 waliachwa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Msekela (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa benki hiyo, Tully Mwambapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watu wenye ulemavu wahakikishiwa fursa

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imesisitiza itaendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kuwajumuisha watu wenye ulemavu katika nyanja zote za uchumi.

Aidha, imetoa wito kwa wadau kutoa mchango wao katika kuwawezesha watu wenye ulemavu hususan watoto ili waweze kupata elimu na malezi bora yatakayowawezesha kutimiza ndoto zao kwa kutoa mchango wao katika maendeleo ya nchi.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Masuala ya Watu Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, mwishoni mwa wiki alipokuwa akikabidhi vifaa vya msaada katika shule tatu za watu wenye ulemavu ambavyo vimetolewa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 15 ambao ulihusisha ukaguzi wa usalama na afya hususan katika mabweni ya wanafunzi, umetolewa katika shule za msingi za watoto wenye ulemavu za Uhuru Mchanganyiko ya Ilala (Dar es Salaam), Mazinyungu ya Kilosa (Morogoro) na Buigiri ya Chamwino (Dodoma).

Miongoni mwa vifaa vilivyotolewa ni kompyuta, vifaa vya kuzimia moto, taulo za kike, vifaa kinga, vifaa vya usafi, karatasi na vibao maalum ya kuandikia watu wenye ulemavu.

Alisema watoto wenye ulemavu wana uwezo mkubwa ambao hautofautiani na watu wasiokuwa na ulemavu, hivyo endapo watalelewa vizuri na kupata elimu stahiki wanaweza kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa.

"Niwashukuru OSHA kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kufanya ziara katika shule tatu za watoto wenye ulemavu. OSHA imekuwa ni taasisi ya faraja sana kwa watu wenye ulemavu kwani katika kile kidogo wanachokipata wameona ni vema wakashirikiana nami na Ofisi nzima ya Waziri Mkuu kuja kuwatembelea hawa watoto. Hivyo, binafsi nimefarijika sana," alisema na kuongeza:

"Natamani kuona watu wenye ulemavu wanajumuishwa ipasavyo katika sekta zote na ndio maana nimekuwa nikipita katika maeneo mbali mbali ikiwamo ajira, elimu, afya, uchumi ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata nafasi katika kila fursa inayotokea na katika mipango mbali mbali ya serikali."

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema serikali itaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo zikiwemo taasisi, asasi zisizo za kiserikali, kampuni na watu binafsi katika kuwawezesha watu wenye ulemavu ili nao waweze kutoa machango wao katika kuijenga nchi yao.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema msaada huo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa taasisi yake wa kusaidia jamii kwenye sekta za elimu, afya, majanga na uboreshaji wa mazingira ya kazi.

"Sisi tumekuja katika shule hizi za watu wenye ulemavu kwa ajili ya kutoa faraja kwa wanafunzi na watumishi wenzetu ambao wanafanya kazi katika mazingira yenye changamoto nyingi na vihatarishi vingi vikiwamo vihatarishi vya kisaikolojia hivyo wanahitaji kutiwa moyo ili waendelee kuifanya kazi hii ambayo kimsingi ni kazi kubwa na muhimu sana katika maendeleo ya taifa letu," alisema Mwenda.

Wanafunzi na viongozi wa baadhi ya shule zilizopatiwa msaada wa vifaa hivyo, waliishukuru OSHA kwa msaada uliotolewa na kuwaomba wadau wengine kuendelea kusaidia kutatua changamoto zinazokabili shule za watoto wenye ulemavu.

"Binafsi nimefarijika sana kwa sababu sikujua kuwa OSHA watakuja kwani walinipigia tu simu wakiniuliza changamoto tulizonazo, hivyo namshukuru sana Naibu Waziri Ummy ambaye kwa kushirikiana na OSHA wameona waje watutembelee na kutuletea zawadi," alisema Kajika Gallan, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mazinyungu.

# Wahandisi washauri waonyeshwa fursa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, amewataka wahandisi washauri kuchangamkia fursa zinazotolewa katika miradi ya kielelezo nchini, ili kukua kitaaluma na kukuza uchumi wa Taifa.

Alitoa rai hiyo wakati akifungua mkutano wa 35 wa mwaka wa wahandisi washauri ulioandaliwa na Umoja wa Wahandisi Washauri (ACET), mkoani Dar es Salaam uliobeba kaulimbiu ya uhusikaji wa wahandisi washauri wazawa katika miradi ya kielelezo.

Dk. Chamuriho alisema: "Kuhusika kwa wahandisi washauri katika miradi kunasaidia kuendana na Dira ya Taifa ya mwaka 2020-2025 ya kuwa Taifa la Uchumi wa kati wa chini kwa miaka mitano kabla ya wakati wake."

Aliongeza: "Mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yanahusishwa na ninyi wahandisi kwani miradi hii ndiyo inayoleta mafanikio makubwa katika uendelezaji wa miundombinu ambayo ndiyo chachu ya ukuaji wa uchumi."

Alisema ni jukumu la wahandisi kuhakikisha miradi mikubwa ambayo ni ya kielelezo inatendewa haki kwa weledi na kuzingatia thamani ya fedha, ili kuleta tija kwa taifa na kuwawezesha kupata fursa zaidi katika miradi inayotekelezwa nchini.

Aidha, aliwakumbusha wahandisi hao kuwa sayansi na teknolojia vinakuwa kwa kasi, hivyo ni jukumu lao kuhakikisha wanajijengea uwezo ili kuendana na kasi hiyo kwa kuhudhuria kozi mbalimbali zinazotolewa ndani na nje ya nchi.

Kuhusu changamoto za kutoaminiwa katika utekelezaji wa miradi mkubwa, Dk. Chamuriho alisema serikali imeweka sera yenye mambo makuu matatu ambayo ni kujenga uwezo wa upatikanaji wa masoko, kupiga chapuo kwanye teknolojia ili kukuza makandarasi wazawa.

"Sera hii ya ndani inawezesha makandarasi wa nje kuwahusisha makandarasi wa wazawa ili kuweza kuwainua hivyo hakikisheni mnazijua sera hii ya ndani, Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na kanuni zake ili muweze kuzitekeleza," alisema Dk. Chamuriho.

Alisema ili kuwafanya wahandisi washauri waweze kuaminiwa zaidi ni vema wakajiunga ili kuweza kutengeneza kampuni kubwa zenye uwezo wa kutekeleza miradi kwa weledi zaidi.

Naye Rais wa ACET, Mhandisi Deogratius Mugishagwe, aliiomba serikali kuhakikisha wahandisi wanahusishwa katika mpango wa maendeleo wa serikali wa miaka mitano pamoja na kuwawezesha kulipwa kwa wakati kwa kupanga miradi inayotekelezwa kwa kufuata vipaumbele.

Alisema changamoto kubwa wanazokabiliana nazo ni pamoja na kuingiliwa na watu wasiokuwa na ujuzi wa fani, kuchelewa kwa malipo.

Mugishangwe alisema ACET wanachokifanya ni kuhakikisha wahandisi washauri wanajengewa uwezo kila wakati ili waweze kuwa na uwezo wa kushindana na wahandisi washauri kutoka nje ya nchi.



Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula (kushoto), akibadilishana mawazo na Meneja wa Barrick nchini, Georgia Mutagahywa (kulia), wakati wa warsha ya ushirikishwaji wa Watanzania katika mnyororo wa uchumi wa madini iliyoandaliwa na Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited iliyofanyika katika mgodi wa Barrick North Mara mwishoni mwa wiki, (katikati) ni Kamishna wa Madini Tume ya Madini, Janeth Lekashingo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachangishana fedha kuwanusuru wajawazito

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKAZI wa Kijiji cha Bukoba Kata ya Isageje Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wamechangisha Sh. milioni 8.9 na kujenga zahanati ya kijiji ili kuwanusuru wajawazito kutembea umbali wa kilomita 14 kwenda zahanati ya Isagehe kupata huduma za afya ya uzazi.

Kijiji cha Bukoba kina zaidi ya wakazi 2,500 na kila kaya ilichangia vifaa vya ujenzi, fedha na kujenga boma la zahanati huku wakichangiwa Sh.milioni 35, fedha kutoka serikali kuu na mpaka zahanati hiyo inakamilika itagharimu Sh. milioni 61.

Akitoa taatifa ya ujenzi wa zahanati hiyo kwa lamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) Wilaya ya Kahama, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Henry alisema wananchi wanaendelea na michango kwa ajili ya kujenga nyumba ya mganga karibu na zahanati hiyo.

Alisema, kukamilika kwa zahanati hiyo itasaidia pia kutoa huduma kwa wananchi wa vijiji vya Igusule, Mweka na Maluge, na kwamba kazi zilizobakia ni ujenzi wa shimo la kutupa kondo la nyuma, ujenzi wa kichomeo taka na ukamilishaji wa choo cha nje kwa ajili ya wagonjwa watakaofika kupata huduma.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Mohamed Ramadhani, alisema, lengo la kuhamasishana na kujenga zahanati hiyo ni kuwanusuru wajawazito kutembea umbali wa kilometa 14 kwenda na kurudi zahanati ya Isagehe, huku wengine wakitishia kujifungulia njiani.

Mkazi wa kijiji hicho, Matha Yohana, alisema, wamekuwa wakivamiwa na vibaka wakiwa na silaha nyakati za usiku wanaposafirisha mgonjwa kwenda Zahanati ya Isagehe na kunyang'anywa pikipiki au baiskeli, hivyo kukamilika kwa zahanati hiyo kutasaidia kuondoa changamoto hiyo.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kahama, Dk. Lucas David, alisema kwa mwaka huu wa fedha halmashauri imetenga Sh. milioni 281 kwa ajili ya kununua vifaa tiba na thamani za ndani katika zahanati tatu za Iponya, Bukooba na Zahanati ya Ngulu.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 100 zitatumika kufunga mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika zahanati hizo na Sh. milioni 181 zitatumika kununua vifaa tiba na dawa, na kwamba mwezi huu zahanati hizo zitakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

# Sababu Mkombozi kupata faida bil. 3/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara Mkombozi imetangaza kupata ya Sh. bilioni 3.8 baada ya kodi kwa kipindi cha mwaka 2020, huku ikisema sababu ni utekelezaji wenye mafanikio wa mpango wa kuongeza mapato na usimamizi wa gharama.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano huu mkuu wa mwaka wa wanahisa wa benki hiyo, Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Marcellina Chijoriga, alisema ni mafanikio kutokana na benki kupata hasara ya Sh. bilioni 6.5 kwa mwaka 2019.

"Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wenye mafanikio wa mpango wa kuongeza mapato na usimamizi wa gharama," alisema.

Prof. Chijoringa alisema kuongeza kwa faida kwa mwaka 2020 pia kulitokana na kuongezeka kwa amana za wateja ambapo kwa mwaka tajwa ziliongezeka kwa asilimia 14.

"Haya ni matokeo ya utekelezaji mzuri wa mkakati wa soko," alisema huku akiongeza kuwa mikopo na karadha kwa wateja ilipungua kidogo kwa asilimia moja na hivyo ikawa ni moja ya sababu ya kuchangia hesabu nzuri kwa mwaka 2020.

Ili kuendelea kujiimarisha vizuri kwenye soko, Prof. Chijoringa alisema benki itawekeza kwenye mfumo wa dijitali ambao utahusisha shughuli za benki kwa njia ya uwakala, shughuli za benki kwa njia programu ya simu za mkononi, shughuli za kiBenki kwa njia ya intaneti, na mifumo ya malipo.

Kwenye changamoto ambazo benki ilipitia kwa mwaka huo, Thomas Enock, Ofisa Mwendeshaji wa Shughuli za Benki, alisema ni upungufu wa mtaji ambapo benki iliendesha shughuli ikiwa na changamoto kubwa ya mtaji iliyozuia matarajio ya ukuaji wetu kwa mwaka 2020, kutokana na ukomo wa uwezo wa kuwekeza.

Enock aliongeza kuwa janga la COVID-19 pia ilikuwa ni changamoto ambapo benki iliathiriwa sana kutokana na kushuka kwa shughuli za kiuchumi. "Tumeweka mipango yetu ya utekelezaji wa shughuli zetu ili kupunguza madhara kwenye biashara yetu," alisema.

Kuhusu mpango mkakati wa baadaye, alisema kipaumbele kwa sasa ni kushughulikia changamoto zinazoikabili zikiwamo utoshelevu wa mtaji ambao unaunda msingi wa utekelezaji wa mpango mkakati wa siku zijazo.

Nipashe
Spotika



NYOTA 10 WA DARAJA LA DUNIA WALIOSHINDWA KUNG'ARA EPL- UK. 12-13



# KLABU ANAZOWEZA KUTUA KOULIBALY

**NAPLES, Italia**

NAPOLI imethibitisha kwamba, mlinzi wake wa kati, Kalidou Koulibaly anapatikana katika kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto, lakini cha kushangaza klabu chache zinaonyesha kujali.

Kwa kipindi cha misimu michache iliyopita, Koulibaly amekuwa mmoja wa walinzi wanaotakiwa sana katika sayari hii, lakini ada yake ya pauni milini 100 mara zote imekuwa tatizo. Sasa hata hivyo, thamani yake imeshuka hadi pauni milioni 35, maana yake kwamba kuna uwezekano wa kumuuza.

Hapa ngoja tuangalie klabu sita ambazo Koulibaly anaweza kutua kipindi hiki cha majira ya joto.

**6. Liverpool**

Miezi 12 iliyopita, mashabiki wa Liverpool walikuwa wanapiga kelele wakitaka Virgil van Dijk aungane na Koulibaly. Lakini siku hizi kelele hizo ni kama zimekoma.

Koulibaly bila shaka ni mmoja wa walinzi bora duniani, lakini umri wake wa miaka 30 na thamani yake inaonyesha kuwa ghali zaidi. Lakini sasa Liverpool wanaweza kuingia mfukoni na kumsajili kwa ajili ya kuimarisha safu yake ya ulinzi.

**5. Man City**

Manchester City walimhitaji Koulibaly miezi 12 iliyopita, lakini badala ya kulipa kiasi kikubwa cha fedha, wakaamua kumsajili kinda wa Ureno, Ruben Dias.

Unaweza kusema klabu hiyo pengine wana furaha na uamuzi wao huo.

Kwa uhakika wanaonekana kutohitaji tena kumsajili Koulibaly, ingawa ni wazi kwamba wanahitaji kuimarisha safu yao ya ulinzi, kama Aymeric Laporte au Nathan Ake - mmoja wao akaamua kuondoka.

**4. Man United**

Kama huu ungekuwa mwaka 2018, Manchester United pengine tayari wangeshamsajili Koulibaly.

Bahati mbaya ni kwamba Mashetani Wekundu hao kwa sasa hawafikiri tena kuhusu majina makubwa. Wamekuwa wakimfikiria mlinzi kijana, kama Jules Kounde au Pau Torres, lakini tayari wameshamnyaka Raphael Varane.

Lakini bado wana nafasi ya kumwongeza Koulibaly kwenye kikosi chao.

**3. Chelsea**

Chelsea nao walikuwa na nia kubwa ya kumsajili Koulibaly, kwani ni wazi safu yao ya ulinzi ilionekana kipwaya.

Na kwa sasa raia huyo wa Senegal anaweza asiwe kipaumbele chao, lakini anaweza kuwafaaa kwenye mipango yao kama Thomas Tuchel atakuwa na mpango wa kuimarisha kikosi chake hasa safu ya ulinzi.

Kwa sababu Chelsea ina wachezaji wengi vijana, ujio wa Koulibaly utasaini kuimarisha safu ya ulinzi hasa kutokana na uzoefu wake.

**2. Everton**

Kunashaka kubwa kuhusu majaliwa ya Yerry Mina, pamoja na Michael Keane, hivyo Everton lazima waingie sokoni kwa ajli ya kutafuta mlinzi na kocha, Rafa Benitez kwa namna yoyote akili yake itakuwa kwa Koulibaly.

Koulibaly anaweza kuwa msaada mkubwa kwa Toffees hao ili kuziba pengo la Mina ana Keane ambao kwa namna yoyote wanaonekana wanaondoka.

Kwa kiasi cha fedha ambayo sasa Koulibaly anauzwa inaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho na hivyo atawasaidia zaidi.

**1. PSG**

PSG imeonyesha ishara yao ya kutaka walinzi bora kwenye kikosi chake msimu huu.

Tayari wamemsajili mlinzi wa kulia, Achraf Hakimi ambaye sasa atacheza sambamba na Sergio Ramos aliyetua hapo akiwa mchezaji huru kutoka Real Madrid.

Kumbuka pia wana mtu kama Marquinhos ambaye amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi hicho.

Ingawa Presnel Kimpembe naye ni bora na anauwezo mkubwa kwenye majukumu yake, lakini PSG wanaweza pia kumfikiria Koulibaly ikiwa ni sehemu tu ya kuimarisha zaidi safu yao.

Fedha sio tatizo kwa PSG, kwani wanauwezo wa kutoa kiasi chochote kitakachohitajiwa na kwa vyovyote, atakuwa nguzo imara kwa kikosi hicho msimu huu.

## ISIKUPITE

ARSENAL inajiandaa kumpa ofa ya mkataba mpya kiungo wake, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 28, ambaye awali alikuwa anahusishwa na mpango wa kuuzwa kutoka hapo kwenye dimba la Emirates lililoko London Kaskazini nchini England.



## Extra Time

# NYOTA 10 WA DUNIA WALIOFELI KUNG'ARA EPL




DI MARIA

**LONDON, England**

LIGI Kuu ya England, EPL, inavutia wachezaji wengi wenye vipaji vya daraja la dunia, lakini huwa ni sehemu katili zaidi kwa vipaji vyao kwa baadhi ya wachezaji.

Raphael Varane ni mchezaji wa hivi karibuni sana ambaye ameamua kwenda kucheza Ligi Kuu ya England akitokea Real Madrid na kutua pale Manchester United.

Na ingawa mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa ana kila aina ya ubora pamoja na uzoefu wa kutosha kuweza kuwasaidia Mashetani Wekundu hao, lakini anaweza kujikuta akishindwa kung'ara kwenye ligi hiyo.

Makala haya ya 90min.com yanawaangalia wachezaji 10 wa daraja la juu duniani ambao walishindwa kuonesha viwango vyao kwenye ligi Kuu England, licha kule walikotaka kuwa kwenye kiwango bora sana.

**10. Davor Suker**

Mshindi wa LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid, na mshindi wa kiatu cha dhahabu kwa ufungaji bora wa mabao katika fainali ya michuano ya Kombe la Dunia mwaka 1998 na mshindi wa pili kwenye tuzo za Ballon d'Or mwaka huo huo, Davor Suker akawasili Arsenal mwaka 1999 huku wengi wakimatarajia kufanya makubwa sana.

Raia huyo wa Croatia alifunga mabao nane kwa washikabunduki hao kwenye Ligi Kuu katika msimu mmoja tu aliocheza hapo, kabla ya Harry Redknapp kumchukua kule West Ham, ambako alifunga mabao mawili.

**9. George Weah**

George Weah ni gwiji hasa kwa kile alichokifanya kule Paris Saint-Germain na AC Milan. Kiwango chake kule PSG kilimuwezesha kushinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka 1995, kabla ya kwenda kufanya makubwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akiwa na Milan.

Kwa kipindi cha misimu minne akashinda taji la ligi mara mbili na Weah akaondoka Italia kwenda Chelsea, Januari 2000 kwa mkopo, lakini alifunga mabao matano.

Na baadaye Milan wakamwachia kwenda Manchester City kwa mkataba wa kudumu, ambako alifunga bao moja kwenye ligi.

**8. Deco**

Ilikuwa ni burudani kumwona akicheza katika kiwango chake bora, Deco alikuwa mmoja wa viungo bora zaidi ambao waliofanya mchezo wa soka kuonekana rahisi sana.

Lakini aliposajiliwa Chelsea kutoka Barcelona kuelekea msimu wa 2008/09, Blues hao walikuwa na imani nae kubwa sana. Alitoa asisti na kufunga bao la umbali wa yadi 30 katika mchezo wake wa kwanza kuichezea Chelsea kwenye Ligi Kuu dhidi ya Portsmouth.

Bahati mbaya, Deco akajikuta kiwango chake kikiporomoka na msimu huo raia huyo wa Ureno alifunga mabao matatu na kutoa pasi za mabao mbili.

Mwaka uliofuata, Deco akatwaa taji chini ya kocha, Carlo Ancelotti, lakini akakosa namba na hivyo akaondoka na kwenda kujiunga na Fluminense ya Brazil.

**7. Gonzalo Higuain**

Kwa mchezaji aliyeweza kufunga mabao 76 kwenye Serie A kutoka mwaka 2015 hadi 2018, Gonzalo Higuain akaenda kwa mkopo Chelsea, Januari 2019.

Raia huyo wa Argentina alifunga mabao matano katika mechi 19 alizocheza na akaonekana hafiti kwenye mfumo wa Chelsea.

6. Maicon

Pengine ni mlinzi bora zaidi wa kulia wa mwaka 2010, Maicon alikuwa hashikiki wakati akitamba kule Inter Milan na timu ya taifa ya Brazil kwa zaidi ya muongo mmoja.

Raia huyo wa Brazil anakumbukwa kwa bao alilofunga kwenye mchezo wa kombe la Dunia mwaka 2010 dhidi ya Korea Kaskazini - na Manchester City wakamchukua.

Wengi walitarajia makubwa kutoka kwake wakati akitua hapo City mwaka 2012, hata hivyo, Maicon muda wake pale Etihad ulikuwa mbaya, alicheza mechi tisa za Ligi bila kuwa na bao wala asisti na akahamia Roma baada ya msimu mmoja tu.

**5. Fernando Morientes**

Straika ambaye mara zote alikuwa anafunga kwenye mechi za LaLiga, Fernando Morientes na akahamia Liverpool msimu wa 2004/05 akitoka kushinda mataji mawili ya Ligi na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid.

Katika umri wake wa miaka 28, alikuwa anatarajiwa kuwa mchezaji ambaye atakuwa kwenye ubora wa juu kabisa.

Hata hivyo, alipata nafasi ya kucheza mechi nane za Ligi Kuu England kwa kipindi cha misimu miwili. Na baada ya kushindwa kuonesha kiwango cha juu Mashetani Wekundu wakamwachia raia huyo wa Hispania kwenda Valencia.

**4. Juan Sebastian Veron**

Mshindi wa kombe la UEFA, bingwa wa Serie A na mshindi mara mbili wa kombe la Coppa Italia kabla ya kutua England mwaka 2001, Juan Sebastian Veron alikuwa ni kiungo aliyekamilika.

Kutokana na uwezo wake dimbani pamoja na kasi na nguvu kwa raia huyo wa Argentina, Sir Alex Ferguson akaatoa pauni milioni 28 kwa Lazio na kumleta kwenye soka la Uingereza wakati akiwa kwenye kiwango chake bora kabisa. Mwanzoni, Veron alionesha imani kwamba, atakwenda kulipa fadhira ya kuaminiwa, akishinda tuzo ya mchezaji bora wa mwezi (Septemba).

Hata hivyo, tofauti na matarajio akashindwa kufiti pale Old Trafford na akajikuta akitua Chelsea kipindi cha majira ya joto mwaka 2003.

Nako akashindwa kutamba na Veron akajikuta akirudi nchini Italia kuichezea Inter Milan.

**3. Angel Di Maria**

Mmoja wa washambuliaji bora kabisa, Angel Di Maria, lakini akajikuta kwenye wakati mgumu sana mara baada ya kutua Manchester United akitokea Real Madrid kuelekea msimu wa 2014/15.

Alitengeneza pasi za mabao 11 kwenye Ligi, lakini akafunga mabao matatu kwenye ligi na hivyo kushindwa kuthibitisha thamani yake ya pauni milioni 59.7 aliyosajiliwa kutokea Madrid, ada iliyoweka rekodi kwenye soka la Uingereza.

Baada ya kumalizika kwa msimu, gazeti la Daily Telegraph likamchagua Di Maria kuwa ndio usajili wa hovyo zaidi kwa msimu, na akaondoka pale Old Trafford na kutua PSG.

**2. Radamel Falcao**

Mmoja wa wachezaji ambaye alikuwa anatajwa kuwa dunia ya soka itakuwa miguuni mwake ni Radamel Falcao kutokana na kiwango alichokionyesha kule Atletico Madrid na Monaco mwanzoni mwa miaka ya 2010.

Raia huyo wa Colombia akaamua kwenda kujijaribu mwenyewe nchini England, wakati alipotua Manchester United kwa mkopo msimu wa 2014/15.

Falcao alifunga mabao manne katika mechi 26 za Ligi Kuu kabla ya kuondoka na kurudi zake Monaco.

Falcao alirudi tena England kujiunga na Chelsea kwa mkopo ambako alikuwa na msimu mbaya zaidi, akifunga bao moja kwenye mechi za mashindano yote.

**1. Andriy Shevchenko**

Bila shaka yoyote alikuwa kwenye kiwango cha juu mno, Andriy Shevchenko alishinda tuzo ya Ballon d'Or miaka miwili kabla ya kuhamia Chelsea kipindi cha majira ya joto mwaka 2006. Na kwa sababu Roman Abramovich (mmiliki wa Chelsea) alikuwa akiwania saini ya straika huyo wa miaka mingi, hatimaye dili likakamilika.

Gwiji huyo alifunga mabao tisa katika mechi 47 za Ligi Kuu.

Mfungaji huyo wa muda wote kwa kikosi cha timu ya taifa ya Ukraine na mfungaji namba mbili wa muda wote kule AC Milan alimaliza muda wake wa kucheza pale Stamford Bridge baada ya mwaka mmoja na nusu, na akarudi Rossoneri kwa kipindi cha pili msimu wa 2008/09 kabla ya kuhamia Dynamo Kiev alikostaafia soka.

## Nukuu


"KWAHIYO wachezaji wapya tutakaowasajili hawatazidi watano au sita kwa ajili ya kuboresha maeneo hayo yaliyoainishwa." **Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli.**



"NI kweli mkataba wangu unaelekea mwisho. Utamalizika mwezi ujao (huu) na hili ni jambo la kawaida kwa kocha yoyote yule. Kama watanihitaji sawa, lakini kama hawanitaki, basi tutapeana mkono wa kwaheri, lakini mpaka muda huu mimi ni kocha wa Coastal Union na muda ukifika ndiyo tutaongea." **Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda.**



"Gerald Mdamu alipata ajali akiwa na basi la timu wakiwamo wachezaji wengine, ila mshambuliaji huyo ndio aliyeumia sana, sio ukweli kuhusu kukatwa mguu na matibabu yanaendelea vizuri." **Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Polisi Tanzania, Robert Munisi.**





Wallace Karia

# VIONGOZI 7 WALIOONGOZA SOKA LA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA inatarajia kupata kiongozi wa soka Agosti 7, kwenye Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika jijini Tanga.

Rais Wallace Karia ndiye mgombea pekee aliyebaki na anayetarajiwa kupigiwa kura na wajumbe ambao watakuwa halali kupiga kura Jumamosi ijayo.

Ikumbukwe kuwa Kamati ya uchaguzi wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) chini ya Mwenyekiti wake, Wakili Kiomoni Kimamba na Makamu wake Benjamin Kalume, iliwaengua baadhi ya wagombea wa urais wa shirikisho hilo, kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu.

Awali kabisa iliwaengua wagombea Ally Mayay, Oscar Oscar na Ally Salehe, huku kwenye nafasi ya Kamati ya Utendaji, Saady Kihmji na Jimmy Kindoki, majina yao pia yalifyekwa kwa sababu mbalimbali.

Wakapitishwa Rais anayetetea kiti chake, Karia, Hawa Mninga na Euvance Mgeusa.

Mwishoni mwa mwezi Juni, Mninga na Mgeusa nao pia wakafyekwa kwa kutokidhi vigezo vyote vinavyotakiwa.

Hapo ndipo Karia alipobaki kuwa mgombea pekee kwa kukidhi vigezo vyote vinavyotakiwa.

Kwanza kabisa utaanza Mkutano Mkuu wa TFF, ambapo moja ya Ajenda ya mkutano huo ni uchaguzi wa kuchagua viongozi wa shirikisho hilo ikiwamo nafasi ya urais na nafasi sita (6) za wajumbe wa kamati ya utendaji.

Iwapo Karia ataingia madarakani, basi ataendelea kuwa kiongozi wa saba kuliongoza soka la Tanzania tangu mwaka 1967.

Yeyote atakayeukwaa urais wa TFF nje ya Karia, basi atakuwa ni kiongozi wa nane wa shirikisho hilo, tangu kikiitwa Chama cha Soka Tanzania (FAT).

Kwenye makala hii tumewaorodheshea viongozi wote waliowahi kuongoza mpira wa Tanzania kwenye ngazi ya juu.

Kabla ya hapo tuangalia historia ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), ambalo zamani lilikuwa Chama cha Soka cha Tanzania (FAT), ni chombo kinachotawala mpira wa miguu nchini Tanzania na inasimamia timu za taifa za mpira wa miguu za Tanzania. TFF kirefu chake ni 'Tanzania Football Federation'.

Lilianzishwa mwaka 1930 na ina uhusiano na FIFA tangu mwaka 1964.

Shirikisho hilo lilianzishwa kama Chama cha Soka Tanganyika (TFA). Baadaye ilipewa jina kama Chama cha Soka cha Tanzania (FAT) hii ilikuwa mnamo 1971 baada ya marekebisho makubwa katika katiba yake.

FAT ilikuwapo hadi mwaka 2004 wakati jina mpya TFF lilipoanza kutumika baada ya mkutano mkuu uliofanyika tareheDesemba 27, mwaka huo huo. Katiba ya sasa ya TFF ilianza kutumika tarehe 15 Januari 2006 kufuatia Mkutano Mkuu uliofanyika jijini Dar es Salaam Januari 14 - 15, 2006.

Hawa ndiyo viongozi waliowahi kuongoza soka Tanzania kwenye ngazi ya juu, tangu wakati huo ikiitwa (FAT).

**1. Ally Chambuso**

Huyu aliingia kwenye madaraka ya kuliongoza soka la Tanzania mwaka 1967, wakati huo Chama cha Soka kikiitwa (TFA), yaani Chama cha Soka Tanganyika. Mwenyekiti huyu ndiye aliyekuwa ndani ya mabadiliko yaliyotoka kwenye TFA hadi kuwa Chama cha Soka Tanzania (FAT) mwaka 1971.

Ally Chambuso, aliliongoza soka la Tanzania hadi mwaka 1974, hivyo alidumu kwenye uongozi kwa miaka saba.

**2. Said El Maamry**

Ni mmoja kati ya kiongozi maarufu zaidi na wa mfano kwenye historia ya soka la Tanzania.

Aliingia kwenye uongozi mwaka 1974 akichukua nafasi ya Chambuso. Said El Maamry alidumu kama Mwenyekiti wa FAT kwa miaka kumi na tatu, kwani alikiongoza chama hicho hadi mwaka 1987.

Ndiye anashikilia rekodi ya kuwa kiongozi wa juu waliyeongoza soka kwa muda mrefu zaidi mpaka sasa. Alifariki dunia hivi karibuni, Julai 23 mwaka huu, akiwa na miaka 86.

**3. Mohamed Mussa**

Alikuwa Mwenyekiti wa FAT kwa miaka mitano tu. Aliliongoza soka la Tanzania kuanzia mwaka 1987 hadi mwaka 1992. Ni mmoja wa viongozi walioongoza soka nchini kwa muda mfupi.

**4. Muhidini Ndolanga**

Anakumbukwa kama mmoja wa viongozi wa soka la Tanzania aliyekuwa na misimamo mikali na isiyoyumba.

Ndolanga aliingia kwenye madaraka ya kuliongoza soka mwaka 1992 akichukua nafasi ya Mohamed Mussa. Ni mmoja wa viongozi walioshika rekodi ya kuliongoza soka kwa muda mrefu, akizidiwa mwaka mmoja tu na El Maamry.

Alikuwa Mwenyekiti wa FA kwa miaka 12 hadi mwaka 2004.

**5. Leodgar Tenga**

Huyu ni nahodha wa zamani wa klabu za Yanga, Pan African na Timu ya Taifa, Taifa Stars miaka ya 1980.

Aliingia kwenye wadhifa wa kuongoza soka la Tanzania kama Mwenyekiti mwaka 2004, lakini ndiye aliyefanya mabadiliko ya chama hicho kutoka kuwa FAT na kuwa shirikisho, hivyo ikaitwa TFF.

Pia yakafanyika mabadiliko ya Katiba, ambapo pamoja na mambo mengine, mwenyekiti akatambulika kwa cheo cha Rais wa Shirikisho, yeye mwenyewe Tenga akiingia kwenye vitabu vya kumbukumbu ya kuwa Rais wa Kwanza wa TFF. Aliongoza kwa muda wa miaka tisa hadi 2013.

**6. Jamal Malinzi**

Mwaka 2013, ikawa zamu ya Jamal Malinzi. Aliingia madarakani akichukua kijiti kutoka kwa Tenga.


Hata hivyo, ndiye anashikilia rekodi ya kuongoza kwa kipindi kifupi zaidi, kwani mwaka 2017 alipata matatizo ya kesi, na kushindwa kuendelea kwenye muhula mwingine wa pili, akihudumu kwa miaka minne tu.

**7. Wallace Karia**

Ndiye kiongozi anayeiongoza TFF kwa sasa na tayari yupo kwenye kinyang'anyiro cha kupigania muhula wa pili wa uongozi.

Aliingia TFF mwaka 2017 na mpaka sasa 2021 ana miaka minne tu. Kama akipigwa chini naye ataingia kwenye rekodi ya kuongoza kwa kipindi kifupi, lakini akichaguliwa atandelea kuongoza soka la Tanzania hadi mwaka 2025.

**JE, WAJUA?**



ZLATAN Ibrahimovic ni mchezaji wa kwanza kuzichezea klabu saba tofauti kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini hajawahi kushinda taji hilo. Amezichezea kwa nyakati tofauti Ajax, Juventus, Inter Milan, Barcelona, AC Milan, Paris Saint-Germain na Manchester United.



# Ummy azindua ATM za kondomu

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

SERIKALI imelishauri Shirika la Vijana Tanzania (Tayoa) kusambaza makasha ya kusambazia mipira ya kinga (kondomu) na ATM za mipira hiyo kwenye halmashauri zote 184 nchini kama sehemu ya kuchochea mapambano dhidi ya Ukimwi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, wakati wa uzinduzi wa makasha ya kusambazia kondomu aina ya safari zinazosambazwa na Tayoa sehemu mbalimbali nchini kupitia kampuni yake ya Vijanatz Industries Ltd.

Alisema watu wengi wanaona haya kwenda kununua mipira hiyo madukani kwa hofu kuwa wataonekana wahuni, ubunifu wa Tayoa utasaidia watu wengi kuwa na faragha ya kwenda kununua kinga hiyo.

Alisema angependa kuona makasha hayo na ATM hizo zinasambazwa maeneo yote nchini ili watu wajihudumie wenyewe kwa kuwa kwa sasa baadhi ya watu wanashindwa kwenda kuzinunua madukani kwa hofu ya kuonekana wahuni.

"Nawapongeza Tayoa huu ni ubunifu mkubwa sana kwasababu itasaidia sana watu wengi wanunue kondomu na imekuwa mbaya sana hasa kwa wasichana kwasababu wakinunua mipira hii ya kinga wanaonekana malaya, mimi nawashauri kinadada kwamba mkishindwa kujizuia kabisa kufanya ngono ni heri kuwa na kinga kuepuka mambo mengine," alisema Ummy.

Ummy alisema shirika hilo ambalo mwakani linatimiza miaka 24 halijawahi kupoteza mwelekeo wa malengo yao tangu kuanzishwa kwake kwa kuwa siku zote wamekuwa wakisimamia kupambana na ugonjwa wa Ukimwi ambao alisema bado upo na unaua watu wengi nchini.

"Tayoa nawajua na tumefanyakazi na nyinyi hata kabla sijawa Naibu Waziri na baadaye Waziri, kwa muda wote niliowafahamu nyinyi mwelekeo wenu ni kupambana na ugonjwa wa Ukimwi hivyo nawapongeza kwa msimamo wenu thabiti wa kupambana na janga hili," alisema Ummy.

Aliwaomba viongozi wa serikali kwenye ngazi zote kuipa ushirikiano taasisi hiyo itakapokuwa inasambaza mipira hiyo na kuhakikisha makasha na ATM za mipira hiyo zinatunzwa kwa ajili ya matumizi ya muda mrefu kwenye maeneo yao. Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Tayoa, Peter Masika, alisema hadi sasa wameshasambaza makasha 40,000 katika wilaya 169 nchini na wanatarajia kusambaza mengine 40,000 kwenye maeneo mbalimbali nchini ili kufikisha 80,000.

Alisema wanatarajia kuanza kusambaza mashine 5,000 za kutolea mipira hiyo (ATM) katika miaka miwili ijayo na kwamba makasha watakayosambaza yana pande mbili na yatasambazwa kwenye wilaya zote za Tanzania Bara.

Masika aliwashukuru wafadhili wa shirika hilo ambao ni Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Ukimwi (Global Fund), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Wanawake, Jinsia na Watoto, Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) na Wizara ya TAMISEMI.

Alisema kwa sasa Tayoa kwa kushirikiana na AMREF wanatekeleza mradi wa Global Fund unaowalenga wasichana walio katika umri wa kubalehe na wanawake vijana katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga, Singida na Geita kwani kundi hilo ndilo lililo katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Vijana Tayoa, Peter Masika, akimfafanulia jambo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TAMISEMI, Ummy Mwalimu, namna makasha ya kusambazia kondomu yanavyofanyakazi, mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa makasha hayo jijini Dodoma. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mkuchika atoa neno kwa maaskofu kuhusu rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Ofisi ya Rais Ikulu (kazi maalumu), George Mkuchika, amewataka maaskofu na wachungaji kuacha tabia ya kuendekeza rushwa katika kazi zao za kila siku, badala yake wamtumikie Mungu ili kujenga kanisa bora.

Alisisitiza viongozi wa dini kuwafundisha watoto maadili tangu wakiwa 'Sunday School' ili kuwajengea uwezo wa kutambua nini maana ya maadili wakiwa wadogo.

Aliyasema hayo wakati akitoa mada inayohusu maadili katika mkutano wa Sinodini ya 21 wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT), uliofanyika jijini hapa.

Mkuchika alisema rushwa ni adui wa haki hivyo viongozi wa dini wanapaswa kuipiga vita katika mahubiri yao ya kila siku mbele ya waumini wao.

Mkuchika alisema rushwa katika mikusanyiko inachangia kurudisha maendeleo nyuma, hivyo ili kuleta maendeleo bora kanisani na jamii kwa ujumla, watumishi wa Mungu wanapaswa kupiga vita jambo hilo.

"Viongozi wa dini saidieni kuhubiri suala hili, tunahitaji kuona linakemewa makanisani ili jamii ijue rushwa haitakiwi," alisema.

Akizungumzia suala la maadili, alisema wazazi na walezi wanapaswa kusaidia kuwajengea watoto misingi ya maadili tangu wakiwa wadogo ili kadri wanavyokuwa wajue nini maana ya maadili.

Alisema wakifanya hivyo kwa kushirikiana na mahubiri ya kanisani kwa watoto hao, yatasaidia kuwajengea hofu ya Mungu kwa misingi ya imani ikiwamo kuzingatia utamaduni wa watu.

Alisema mtoto anajifunza kuwa kuomba au kupokea rushwa ni hatari tokea akiwa mdogo, hivyo suala la kujua maadili ni la muhimu kujifunza tokea mdogo.

Askofu wa Kanisa la Anglikan Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, alimshukuru Waziri Mkuchika kwa mada ya maadili aliyoitoa huku akisisitiza wataizingatia ipasavyo katika kazi zao za utume.

Alisema suala la maadili ni muhimu kwa kila mmoja na viongozi wa kanisa hilo waliohudhuria mkutano huo wanapaswa kuzingatia na kwenda kuhubiri katika maeneo yao ya utumishi.

Alisema kanisa hilo limekuwa likisisitiza maadili kwa viongozi, wazazi na walezi ili kuhakikisha waumini wanatambua umuhimu wa maadili wanapokuwa kanisani na sehemu nyingine.

# Wahitimu vyuo ufundi watakiwa kuchangamkia mikopo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WANAFUNZI wanaomaliza vyuo vya ufundi nchini wametakiwa kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na halmashauri kupitia mfuko wa makundi maalumu.

Pia wametakiwa kutumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutangaza biashara zao pamoja na kuongeza ujuzi wa fani walizojifunza.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Jiji la Dodoma Sharifa Nabalang'anya, alitoa kauli hiyo wakati wa hotuba yake ya mahafali ya 83 ya Chuo cha Mafunzo ya Ushonaji cha Young Women's Christian Association (YWCA) cha jijini hapa.

Aliwataka vijana wanaohitimu mafunzo ya vyuo vya ufundi nchini kuchangamkia fursa ya mikopo inayotolewa halmashauri kupitia fedha za mfuko wa makundi maalumu wa walemavu, vijana na wanawake ulioanzishwa na serikali.

"Serikali imeanzisha mikopo hii kwa ajili ya makundi hayo hivyo ninyi wahitimu changamkieni fursa hii ya mikopo inayotolewa ili kuanzisha miradi au kukuza mitaji yenu," alisema.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetenga, zaidi ya Sh. bilioni 2.6 katika bajeti yake ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 kwa ajili ya mikopo ya makundi hayo maalumu.

Alisema katika mikopo hiyo makundi ya kinamama na vijana yanatakiwa kuunda vikundi vya kuanzia watu watano na zaidi na visajiliwe kwenye kata husika.

Pia mikopo kwa upande wa watu wenye ulemavu wanaruhusiwa kukopa kupitia vikundi vyao watakavyounda na kuvisajili au kupitia mtu mmoja mmoja.

Aliwataka waliohitimu mafunzo hayo ya ushonaji kutumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutangaza biashara zao pamoja na kujiongezea elimu ya ujuzi ufundi mbalimbali.

Naomi Mmanyi akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wenzake alisema walipokuwa chuoni hapo walifundishwa elimu ya ushonaji, ujasiriamali, afya ya uzazi pamoja na kupinga mimba zisizotarajiwa.

Alisema wanakabiliwa na changamoto ya vitendea kazi na wakifanikiwa kupata cherehani zao watakuwa na uwezo wa kujiajiri kutokana na ujuzi wa kutosha kushona nguo aina mbalimbali.

Katibu wa Tawi la YWCA Mkoa wa Dodoma, Anna Wami, alifafanua kuwa tawi hilo ni Chama cha Wanawake wa Kikristo Tanzania na ni asasi inayoongozwa na wanawake inayotoa mafunzo ya ushonaji kwa wasichana tangu mwaka 1979 bila kujali itikadi ya dini.

Wami alisema YWCA ina matawi 21 nchini na makao makuu yake hapa nchini yapo mkoani Dar es Salaam.

Alisema lengo la Taasisi hiyo ni kuwajengea uwezo wananwake katika kujikwamua kiuchumi na kijamii na kuchangia katika kuleta haki za binadamu bila kujali itikadi zao za dini.





# Mafunzo ya uanagenzi kunufaisha vijana 14,000

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuzindua rasmi mafunzo ya uanagenzi awamu ya tatu yanayofanyika katika vyuo 72 vya Tanzania Bara, ambapo vijana 14,440 wanatarajiwa kunufaika nayo ili wawe na ujuzi wa kutosha kufanya majukumu yao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi na Watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari ambapo alisema uzinduzi huo utafanyika leo katika Chuo Kikuu cha Sanyansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST).

Alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa miezi sita, na kwamba tangu yalipoanza yamefanyika awamu mbili ambazo ziliwanufaisha jumla ya vijana 28,941 ambao wameshajifunza fani mbalimbali za kukuza ujuzi.

Alisema mafunzo hayo yanamhusisha mhusika kutumia asilimia 40 ya muda anaokuwa chuoni kujifunza kwa nadharia darasani na asilimia 60 ya muda anautumia kwa masomo ya vitendo sehemu ya kazi.

"Mafunzo haya ni sehemu ya progamu yetu ya kukuza ujuzi nchini ambapo mafunzo mengine ni ya uzoefu kazini kwa wahitimu, urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi namafunzo ya kuhuisha ujuzi kwa wafanyakazi," alisema Waziri Mhagama.

Alisema baada ya vijana hao kuhitimu mwezi Desemba mwaka huu idadi ya wanufaika wa programu hiyo ya kukuza ujuzi nchini watafikia 80,320 na hivyo kuwa na nguvu kazi ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi pamoja na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Alisema katika mafunzo hayo vijana hao hawalipii gharama yoyote kwa maelezo kuwa asilimia 100 ya gharama zote inagharimiwa na serikali, hivyo kijana akiombwa chochote na mtu yeyote ili awe miongoni mwa wanufaika hiyo itatafsiriwa kuwa ni rushwa.

Alisema kabla ya kuzindua mafunzo hayo, Waziri Mkuu atatembelea vyuo mbalimbali mkoani Mbeya ambavyo vinatoa mafunzo hayo ambavyo ni Kyela Polytechnic College, Vyuo vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) vya Mbeya na Busokelo, Chuo cha Ufundi cha Magereza na Chuo Kikuu cha MUST.

Alisema baadhi ya vijana hao watatumika kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo miradi ya kimkakati kama reli ya kisasa, bomba la mafuta la Afrika Mashariki na mradi wa bwawa la umeme wa maji wa Mwalimu Julius Nyerere.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kuelekea siku ya uzinduzi wa mafunzo hayo pamoja na ziara ya siku sita ya Waziri Mkuu mkoani humo hali ya ulinzi na usalama ni ya kuridhisha.

Aliipongeza serikali kwa kuanzisha mafunzo hayo, na kwamba yanasaidia kuongeza idadi ya wataalamu nchini, huku akiipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kuamua kufanyia uzinduzi wa mafunzo hayo Mbeya.

"Tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuanzisha mafunzo haya muhimu kwa vijana wetu, yatasaidia sana kukuza ujuzi na niwahakikishie tu kuwa uzinduzi utafanyika katika hali ya amani na utulivu," alisema Homera.

Katika hatua nyingine Waziri Mhagama aliwataka vijana na wageni wengine watakaohudhuria hafla ya uzinduzi wa mafunzo hayo kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona kwa kuvaa barakoa na kuwa na vitakasa mikono.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi na Watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama (katikati) akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), wakati wa kukagua eneo litakalofanyika uzinduzi wa mafunzo ya uanagenzi katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) juzi, kulia ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Aloyce Mvuma. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wafugaji ng'ombe wa maziwa kunufaika bei

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, amewaahidi wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kuanza kunufaika baada ya kuweka mikakati ya kutafuta wawekezaji ambao watanunua bidhaa hiyo kwa bei nzuri ukilinganisha na sasa, ambapo bei ya bidhaa hiyo sio ya kuridhisha.

Dk. Anney aliyasema hayo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambapo ziliibuka hoja mbalimbali kuhusu bidhaa hiyo kuuzwa kwa gharama ndogo, ukilinganisha na ubora wa bidhaa yenyewe.

Miongoni mwa mikakati ya Dk. Anney ni kukamilisha makubaliano ya mwekezaji ASAS pamoja na wadau wengine ambao wanaendelea kuvutiwa na mazingira mazuri ya wilaya hiyo.

"Lita moja ya maziwa huuzwa shilingi 600 na wanaonunua mfano Tanga Fresh wao huuza kwa shilingi 1,200 wakati uzalishaji wa maziwa wilayani Rungwe ni lita milioni 60 hii inaonyesha namna wafugaji wanavyopata hasara na bidhaa hiyo," alisema Dk. Anney.

Aliongeza kuwa hivi karibuni wataongeza ng'ombe wengine wa kisasa ili kuhakikisha bidhaa ya maziwa inapatikana kwa wingi na kutafuta soko la uhakika.

Kuhusu bei ya zao la kokoa, alisema serikali imetoa bei elekezi ya zao hilo ni shilingi 4,200 kwa kilo moja na sio vinginevyo na kuagiza kwa wanunuzi kutofika kwenye vyama vya ushirika, kutokana na tatizo hilo aliahidi kuongea na wawekezaji kuanzisha viwanda ili kuchakata zao hilo na kuongeza thamani ikiwamo utengenezaji wa chokleti.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, alisema msimamo wa Baraza la Madiwani ni kuondoa walanguzi wote wanaowakandamiza wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuendelea kuwashawishi wawekezaji wengine wenye nia ya kuwainua wafugaji.

Alisema baraza kwa kushirikiana na viongozi wa halmashauri wataendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya upatikanaji na uzalishaji wa maziwa bora ili kupata soko la uhakika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Loema Peter, alisema bidhaa ya maziwa imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza mapato, na kwamba wataendelea kuboresha mazingira mazuri ili bei ya bidhaa hiyo iwe nzuri na kunufaisha mfugaji.

# Utafiti wagundua aina mpya mbolea

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imefanya utafiti na kubaini aina mpya ya mbolea ambayo inaweza kumsaidia mkulima wa mahindi kuongeza tija katika uzalishaji na kuinua uchumi wake.

Utafiti huo umefanywa Mbozi, Uyole, Mufindi na Kilolo umegundua hiyo ambayo inaweza kumsaidia mkulima kupata mazao bora na mengi.

Kwa mujibu wa mtafiti wa mbolea kituo cha Uyole, Fredrick Mlowe, utafiti huo unalenga kumsaidia mkulima kutumia gharama ndogo katika uzalishaji na kupata mavuno mengi kulinganisha na ilivyo sasa ambapo bei ya pembejeo za kilimo zinauzwa kwa gharama kubwa.

Alisema baada ya utafiti huo mkulima ataweza kutumia mifuko miwili tu badala ya mitano au minne ambayo alikuwa akitumia awali.

"Tuliamua kufanya utafiti kwa kuzingatia hali ya hewa na udongo kutoka maeneo mbalimbali mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kubuni mbolea bora, ambayo itakuwa msaada mkubwa kwa mkulima kupata mavuno mengi na kwa kuanza tayari wakulima wa Wilaya ya Mbozi, Uyole, Mufindi na Kilolo wamenufaika na ubunifu wetu," alisema Mlowe.

Akizungumzia matumizi ya mbolea hiyo, Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo uyole, Dk. Tulole Bucheki, alisema mkulima atatumia kiasi kidogo cha mbolea ikilinganishwa na mbolea nyingine.

Alisema mbolea hiyo inauweza wa kuongeza uzalishaji wa mahindi kutoka gunia 15 hadi 25 kwa ekari, na kwamba mbolea hiyo inayotumika ina madini yote muhimu yanayohitajika kwa ajili kurutubisha mahindi shambani.

Mmoja wa wakulima, Samuel Sinkonde kutoka Kata ya Uyole, alisema amefanya majaribio mbolea hiyo ambayo inauzwa kwa gharama nafuu, na kwamba ina uwezo wa kuzalisha mavuno mengi.

Naye mwanafunzi wa vitendo katika kituo hicho, Jenista Nyiwili, alisema mbolea hiyo imeleta tija kwa mkulima kwa sababu ina virutubisho vyote muhimu, na kwamba imewapunguzia gharama kubwa wakulima katika uzalishaji.

Alisema jukumu kubwa alilonalo ni kwenda kuwafundisha na kuwahamasisha wakulima matumizi sahihi ya mbolea hiyo ili kuongeza uzalishaji wa mahindi, na kuiomba TARI kusmbaza mbolea hiyo maeneo mbalimbali nchini.



# China yakabidhi chanjo 100,000 Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BALOZI mdogo wa China, Zanzibar, Zhang Zhisheng, amesema nchi yake itaendelea kukisaidia kisiwa hicho dhidi ya vita ya janga la corona na kutoa msaada wa hali na mali kulingana na uwezo wao.

Aliyasema hayo juzi katika kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasili na chanjo 100,000 za corona kwa ajili ya Zanzibar.

Balozi huyo alitoa wito kwa jamii ya mataifa mengine kuendelea kuimarisha juhudi zao za kuiunga mkono Tanzania ikiwamo Zanzibar bila kuweka masharti yoyote katika kupambana na janga la ugonjwa huo.

Alisema mapambano dhidi ya Covid-19 yanahitaji mshikamano na ushirikiano kote ulimwenguni na katika kupambana na janga hilo ni vyema elimu itolewa kuhusu umuhimu wa chanjo ya corona.

"Licha ya uboreshaji wa haraka wa virusi, chanjo ambazo zimepewa leseni na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), pamoja na chanjo zilizotengenezwa na kampuni za Wachina za Sinopharm na Sinovac, zinafaa dhidi ya aina zote za mzunguko ulimwenguni," alisema Balozi Zhisheng.

Alisema chanjo aina ya Sinovac imeshasambazwa ulimwenguni na zaidi ya dozi bilioni 1.3 zimeshatolewa kwa nchi zaidi ya 50.

Balozi huyo alisema vita dhidi ya janga la Covid-19 bado linahitaji njia ndefu na hadi sasa hakuna chanjo ambayo inaweza kuzuia kabisa maambukizi, badala yake inapunguza hatari za kuambukizwa.

"Ninashauri umma ujaribu kadiri uwezavyo kupunguza mikusanyiko wa kijamii usio wa lazima, kuvaa barakoa sote tushirikiane katika kuchukua tahadhari," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Afya baada ya kupokea chanjo hizo, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, aliwataka wananchi kuachana na upotoshaji unaotolewa na baadhi ya watu kuhusu madhara ya chanjo ya corona.

Alisema chanjo hiyo imefanyiwa utafiti wa kisayansi na haina madhara yoyote tofauti na inavyoelezwa kuwa ina madhara na baadhi ya watu wanaotoa taarifa za upoteshaji.

"Chanjo hizi zimefanyiwa utafiti wa kisayansi na zinafaa kwa matumizi ya binadamu katika kupambana na janga la corona na serikali itaendelea kutafuta wadau wengine kupata chanjo na tunaishukuru Serikali ya China kwa msaada huu," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Abdallah Suleiman Ali, alisema yeye ni miongoni mwa watu waliopata chanjo ya corona na hakuna athari yoyote ilijitokeza kwake baada ya kuchanjwa.

Alisema chanjo hizo zilizokabidhiwa zitaendelea kutolewa kwa wahudumu wa afya na sekta ya utalii na baada ya hapo itashuka kwa wananchi watakaochanjwa bure.

Chanjo hizo aina ya Sinovac zilizopokelewa juzi ni msaada wa pili baada ya dozi zingine 10,000 za chanjo zilizotolewa mwezi mmoja uliopita kama msaada wa dharura ulioombwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanziar kwa ajili ya Mahujaji ambao walitarajiwa kwenda kuhiji kabla ya Saud Arabia kusitisha safari za hija nchini humo.

## Thamani ya biashara yaongezeka kwa 14.0%

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

THAMANI ya biashara kwa mwezi Juni 2021, imeonyesha nakisi ya Sh. bilioni 70.7, ikiongezeka kwa asilimia 14.0, ikilinganishwa na Juni 2020 na kwa asilimia 0.3 ikilinganishwa na Mei 2021.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Idara za Takwimu za Kiuchumi Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Abdul-rauf Ramadhan Abeid, alipokuwa akiwasilisha takwimu za biashara za kimataifa kwa mwezi Juni huko Mazizini mjini Unguja.

Alisema, bidhaa zilizosafirishwa zilifikia thamani ya Sh. bilioni 1.9, huku zikipungua kwa asilimia 25.0, ikilinganishwa na mwezi Juni 2020 na kwa asilimia 35.5 ikilinganishwa na mwezi Mei 2021.

Alisema, kundi la vyakula na wanyama hai liliongoza kwa kuchangia asilimia 70.0 ya thamani yote ya usafirishaji wa bidhaa.

Alizitaja bidhaa zilizosafirishwa ni pamoja na mazao ya baharini wakiwamo kamba na kaa, mwani, pumba, mashine na vifaa vya usafirishaji, kemikali, mafuta ya wanyama na mboga, samli na nta. Alisema, usafirishaji wa bidhaa kwa nchi tano zilizoongoza kwa mwezi Juni ulifikia asilimia 81.1 ya thamani ya bidhaa zote zilizosafirishwa, Vietnam iliongoza kwa bidhaa zilizofikia thamani ya Sh. milioni 502.9 sawa na asilimia 26.4.

Juu ya takwimu za uagizaji wa bidhaa, alisema, ziliingizwa bidhaa za thamani ya Sh. bilioni 72.6, ikiwa imeongezeka kwa asilimia 12.5, ikilinganishwa na mwezi Juni 2020 na imepungua kwa asilimia 1.1 ikilinganishwa na Juni 2021.

Naye Mhadhiri Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Estella Ngoma Hassan, alisema, ipo haja ya kuongezewa thamani kwa bidhaa zinazosafirishwa nje ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Alisema, bado hali inaonyesha kuwa vizuri kiuchumi na kuleta faraja kwa wananchi na taifa kwa ujumla na hali hiyo ya nakisi ya biashara imekuwapo hata kwa mataifa yalioendelea kiuchumi.



Balozi mdogo wa China, Zhang Zhisheng (kulia), akizungumza na waandishi wa habari katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume baada ya kuwasili kwa chanjo laki moja za corona zilizotolewa na Serikali ya China. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Makamu wa Pili wa Rais ataka wasanii wathaminiwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amezitaka taasisi mbalimbali na jamii kwa ujumla kuthamini kazi nzuri inayoendelea kufanywa na wasanii nchini kutokana na mchango wao katika kufanikisha maendeleo ya taifa.

Alisema hayo wakati akizindua rasmi tamasha la kwanza la washairi Tanzania lililofanyika jijini hapa.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango wa washairi nchini kutokana na kazi yao nzuri ya kufikisha ujumbe kwa jamii ikiwamo kupinga vitendo vya udhalilishaji, kupiga vita dawa za kulevya pamoja na kutoa elimu kuhusu masuala ya afya.

Alisema mchango huo unaotolewa na wasanii ikijumuisha wasanii wa mashairi na kufanya serikali zote mbili kuunda wizara maalum zinazohusiana na utamaduni, sanaa na michezo katika kuhakikisha kuwa tasnia hiyo inapiga hatua.

"Washairi wamekuwa mstari wa mbele kuisaidia jamii hasa katika kufikisha ujumbe kukemea matendo maovu, kushajiisha ustawi wa wananchi kiafya wakati wa maradhi ya milipuko kama vile kipindupindu, hata janga la Covid-19," alisema Hemed.

Akizungumzia suala la kuhifadhi kazi za wasanii, alizitaka Jumuiya za Hakimiliki COSOTA na COSOZA kusimamia vyema kanuni zilizopo za ukusanyaji wa mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za sanaa ili wasanii wanufaike na matunda ya kazi zao.

Aliyakumbusha mabaraza yanayosimamia sanaa Tanzania kuendelea kuwalea wasanii wa mashairi na sanaa nyinginezo na kuyataka mabaraza hayo kuwawekea mazingira rafiki washairi ili wafaidike kazi zao za sanaa.

Aliwataka washairi kutumia mitandao ya kijamii kama Facebook, You tube, Instagram na tick tok ili kuuza kazi zao na kujikwamua na ukali wa maisha.

Kuhusu changamoto zinazowakabili washairi hao, aliutaka uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha wanakaa pamoja na washairi hao ili kuzimaliza changamoto zote hasa ile ya kukosa ofisi za kudumu huku akisisitiza serikali itaendelea kuikuza sanaa ya ushairi.

Naye Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita aliwapongeza washairi kwa kuandaa tamasha hilo hali iliyosababisha kurudisha hadhi ya mashairi nchini na kuwataka washairi hao kuiga na kusoma kupitia washairi waliotangulia.

Tabia alisema jamii hunufaika kupitia kazi za washairi hasa katika kuelemisha, kukosoa na kuburudisha kutokana na matumizi mazuri ya lugha ya Kiswahili katika kazi hizo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa umoja wa washairi Tanzania (UWASHATA), Hassan Ligile, alisema tamasha hilo litakuwa endelevu kila mwaka ili kurudisha hadhi ya mashairi nchini.

Akisoma risala ya washairi, Said Suleiman Ali, aliiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuziomba taasisi husika za kumbukumbu na historia kuzitambua kazi za washairi na kuzitunza ili kukuza Idara ya Nyaraka, kwa lengo la kuacha athari kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Kupitia tamasha hilo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar amezindua kazi mbalimbali za watunzi wa mashairi kutoka Zanzibar na Tanzania Bara ambazo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa elimu kwa jamii.

# Shule binafsi zatakiwa kutoza ada himilivu

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka wamiliki wa shule binafsi kutoza ada himilivu zitakazowawezesha wazazi wengi kuwapeleka watoto wao shule.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam, Kheri James, kwenye mahafali ya 18 ya Shule ya St. Anne Marie ya Mbezi Kimara.

Alisema iwapo wamiliki wa shule hizo watatoza ada himilivu wazazi wengi watapata uwezo wa kuwapeleka watoto wao kupata elimu hivyo kutoa mchango kwa ukuaji wa sekta hiyo.

"Niwapongeze St. Anne Marie Academy kwa kuendelea kufanya vizuri kitaaluma mwaka hadi mwaka na nimeambiwa mmeongoza Wilaya ya Ubungo na Dar es Salaam miaka minne mfululizo lakini hiki kisiwe kigezo cha kutoza ada kubwa," alisema

"Nimetembelea mazingira ya shule hii yamenivutia sana na nilipofika maktaba ya shule hii nimeona ina kiyoyozi na nimeshangaa kwa mara ya kwanza kuona maktaba ya shule ya msingi ina AC, kweli nimeshangaa na ushamba ukanitoka," alisema.

Mkuu wa shule hiyo, Gladius Ndyetabura, alisema kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka 2017, shule hiyo ilikuwa ya kwanza Wilaya ya Ubungo, ya kwanza Mkoa wa Dar es Salaam na ya nane kitaifa na mwaka 2018 ilikuwa ya kwanza Wilaya ya Ubungo, ya kwanza Mkoa wa Dar es Salaam na ya sita kitaifa.

Alisema mwaka 2019 shule hiyo ilikuwa ya kwanza tena Wilaya ya Ubungo na ya kwanza Mkoa wa Dar es Salaam huku ikishika nafasi ya 13 kitaifa na kwa mwaka 2020 ilikuwa ya kwanza Ubungo, ya kwanza Mkoa wa Dar es Salaam na ya nane kitaifa.

Alisema kwenye matokeo ya mtihani wa moko darasa la saba mwaka huu wanafunzi wote walipata alama A kwenye masomo yote hivyo kuwa ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

# Waliohodhi leseni za uchimbaji kutaifishwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ametoa siku 60 kwa wawekezaji ambao wamehodhi leseni za uchimbaji madini kwa muda mrefu, kuwa watataifishiwa leseni hizo.

Alitoa onyo hilo jana wakati akifunga maonyesho ya biashara na teknolojia ya madini mkoani Shinyanga, na kueleza kwamba serikali imedhamiria sekta ya madini kuwa safi, pamoja na kumaliza migogoro yote ambayo hujitokeza.

Alisema kumekuwapo na tatizo kwa baadhi ya wawekezaji wa madini kuhodhi leseni kwa muda mrefu na kutozitumia, pale yanapovumbuliwa madini na wachimbaji wadogo, ndipo hujitokeza na kudai eneo hilo ni lao.

"Naomba mfikishe salamu kwa wawekezaji wa madini ambao wana leseni za uchimbaji na hawazitumii, tumetoa siku 60 tu zianze kutumika, zaidi ya hapo tunazitaifisha, kutoza gharama ambazo serikali imeingia kutokana kutolipiwa kodi," alisema Biteko na kuongeza:

"Kuhodhi leseni kwa muda mrefu kumesababisha serikali kukosa mapato ya Sh. bilioni tisa, fedha hizi lazima zilipwe hatutakuwa na msalia mtume, hatutaki migogoro ya uchimbaji madini."

Pia, alionya tabia ya utoroshaji madini, kuwataka wachimbaji wauze madini kwenye masoko ya madini, atakaye kiuka kufanya hivyo atachukuliwa hatua kali.

Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula, alikazia suala hilo la utaifishwaji wa leseni za muda mrefu, pamoja na kulipa fedha hizo Sh. bilioni tisa kuwa zitakwenda kusaidia ujenzi wa madarasa, majengo ya afya, miundombinu ya barabara.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alisema maonyesho hayo yamesaidia kuutangaza mkoa huo na kuonyesha fursa za biashara hasa katika sekta ya madini.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (katikati), akizindua Hospitali ya Alexia Toangoma iliyokuwa zahanati na kupandishwa hadhi kuwa hospitali, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Ally Humphrey. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watumishi afya watakiwa kuongeza umakini

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WATUMISHI wa sekta ya afya wametakiwa kuongeza umakini wanapomhudumia mjamzito pamoja na elimu ya afya ya uzazi ili kupunguza ama kumaliza tatizo hilo.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alipokuwa akifungua kikao cha mkoa cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe, chanjo mpya ya Covid-19, huduma za kudhibiti maambukizi ya Ukimwi pamoja na huduma ya afya ya mama na mtoto kilichofanyika mkoani hapa.

Alisema takwimu katika Mkoa wa Mwanza bado ziko juu kwa kuwa mwaka 2020 kulikuwa na vifo 157 na mwaka 2021 hadi mwezi Juni kuna vifo 79.

Aliwataka Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na watoa huduma ya afya waendelee kuwa wamoja katika mapambano dhidi ya vifo vya mama na mtoto kwa kuwa miongoni mwa sababu za vifo hivyo ni pamoja na kutoka damu nyingi wakati wa kujifungua, kifafa cha mimba na uzembe.

Alisema kufanyike tathmini ili kujua kifo kimesababishwa na nini, ili kuwajibishana pale inapotokea uzembe na mambo mengine.

"Kwa ufupi ni kwamba bado tupo kule kule kwa mwaka 2020, vifo 157 na 79 vilivyotokea kwa muda mfupi ni viashiria kwamba hebu tujitathmini sababu ya kila kifo, tukitoa tathmini ya vifo vyote tunaweza," alisema Gabriel.

Alitaka taarifa kamili za wataalamu wa afya katika kila kifo kilipotokea ili kujua sababu zake.

Alisema vijiji vingi havina zahanati na ameishatoa maelekezo kuwa kila Mkuu wa wilaya ahakikishe kila kijiji kinakuwa na huduma hiyo.

"Naamini tutakapokutana ndani ya mwezi mmoja, ningeomba nione mpango kazi mliojiandalia ili kuhakikisha kila kijiji kunakuwa na zahanati kwa kumshirikisha wananchi pale inapowezekana na katikati ya jiji kama kuna mitaa inafahamika kuwa ina maeneo basi wafahamishwe ili kumsaidia mjamzito," alisema Gabriel.

HABARI KIMATAIFA

## Sita wauawa katika shambulio la waasi CAR

**Bangui,** CAR

UJUMBE wa Kulinda Amani wa Umoja wa Mataifa (MINUSCA) katika Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), umesema waasi wa kundi la 3R linalomaanisha Kurejea, Ukombozi na Ukarabati, wamewauwa watu sita na kuwajeruhi wengine kadhaa katika shambulio mwishoni mwa wiki, dhidi ya kijiji cha Mann kilichoko Kaskazini Mashariki

Msemaji wa Ujumbe MINUSCA Luteni Abdoulaziz Fall ameliambia shirika la habari la Ufaransa AFP kwamba waasi hao walifanya mashambulio makubwa, dhidi ya ngome za kijeshi kijijini humo katika saa za alfajiri.

Hakuna habari zaidi zilizotolewa kuhusu sababu za shambulio hilo.

Taifa hilo, kulingana na Umoja wa Mataifa (UN), ni la pili lisilo na maendeleo duniani, bado linaathirika kutokana na matokeo ya mapigano makali ya wenyewe kwa wenyewe yalioibuka mwaka 2013.

**DW**

## Ugiriki yakabiliana na joto kali

**Egion,** UGIRIKI

UGIRIKI inaendelea kukabiliwa na wimbi hatari la joto wakati wazima moto wakiendelea kupambana na moto uliosababishwa na ukame katika maeneo mbalimbali.

Kulingana na kituo cha habari cha serikali, watu 16 walilazimika kutibiwa katika hospitali kwenye rasi ya Peloponnese, Kusini mwa Ugiriki kutokana na matatizo ya kupumua.

Nyumba kadhaa katika eneo la mji mdogo wa Egion ziliharibiwa, hadi jana asubuhi moto huo ulikuwa umedhibitiwa.

Hata hivyo kikosi cha ulinzi wa raia kimeonya kuwa hatari ya moto inabaki juu kutokana na ukame, huku hayo yakiarifia matetemeko mfululizo ya ardhi yametikisa Visiwa vya Dodecanese kusini mashariki mwa Bahari ya Aegean nchini Ugiriki. Hata hivyo hakukuwa na ripoti za uharibifu wa mali au majeruhi.

**DW**



# EABL yaongeza mapato licha ya janga Covid-19

**Nairobi,** KENYA

KAMPUNI ya Bia ya Afrika Mashariki (EABL) Group, imepata ongezeko la mapato la aslimia 15 kufikia shilingi za Kenya bilioni 86.0 kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2021.

Faida kabla ya kodi iliongezeka kwa aslimia mbili, kufikia shilingi bilioni 10.9 na kwamba ukuaji wa faida usioridhisha umechangiwa na gharama za mfumuko wa bei, ubadilishaji wa fedha na gharama za kodi.

Mkurugenzi Mtendaji wa EABL Group Jane Karuku, alisema mwaka wa fedha 2021, umekuwa mgumu kutokana na ugonjwa wa Covid-19 na kuathiri biashara katika eneo lote la Afrika Mashariki.

"Kenya na Uganda ziliweka hatua kali za udhibiti na watu walipunguza matumizi yasiyo ya lazima jambo ambalo liliathiri.

"Tuliweza kukabliana na hali hii kwa kuwekeza kwenye bidhaa, kuongeza uzalishaji na kuendeleza jitihada ili kupunguza matumizi na kuhakikisha tunaendelea kuwa imara," alisema Karuku.

Akizungumzia kuhusu mipango ya mbele Karuku alisema: tunafahamu kuwa athari zinazoletwa na corona zitaendelea. Hata hivyo tuna uhakika kuwa mkakati wetu wunafanya kazi vizuri na tutaendeleza jitihada za kuimarisha biashara."

Alisema kampuni hiyo, imepata mafanikio wakati kuna mazingira magumu ya biashara huku kampuni ikifanya mabadiliko yaliyoendana na tabia zilizobadilika za wateja na biashara kwa njia ya mtandao,

Alisema faida ya EABL baada ya kodi katika kipindi hiki imeshuka kwa asilimia moja kufikia shilingi billion za Kenya Bilioni 7 kutokana na kuathiriwa mfumuko wa bei, kodi na athari za ubadilishaji wa fedha za kigeni.

"Katika kipindi hiki kipaumbele cha kampuni ni kuhakikisha afya na usalama wa watu kwa kuwapatia vifaa vilivyowawezesha kufanya kazi katika mazingira salama."



Maofisa wa Usalama Mji Mkuu wa Ufaransa, Paris mwishoni mwa wiki, walikabiliana na maelfu ya waandamanaji waliokasirishwa na mpango wa serikali wa kuanzisha kibali maalumu kwa waliopigwa chanjo dhidi ya virusi vya corona. **PICHA: DW**

# Ufaransa waandamana kupinga chanjo ya lazima

**Paris,** UFARANSA

MAELFU ya watu waliingia barabarani kupinga hatua ya utoaji wa chanjo ya corona ugonjwa wa Covid-19 kwa lazima kwa baadhi ya taaluma za kikazi na matumizi ya hati ya afya.

Watu hao waliandamana katika maeneo 250 ya nchi, haswa mji mkuu Paris, walijaza viwanja kwa Jumamosi ya tatu mfululizo kupinga sera za serikali za kupambana na Covid-19.

Wafuasi wa yellow vests walikusanyika karibu na kituo cha metro cha Viliers na kuandamana kuelekea Bastille Square wakati wa maandamano yaliyofanyika katika maeneo manne Paris, vikosi vya usalama 3,000 vilitumwa kudhibiti maandamano.

Mvutano ulizuka kati ya polisi na waandamanaji ambao walikuwa wakitoa kauli mbiu kama vile "dikteta gerezani", "uhuru", "Macron ajiuzulu".

Vikosi vya usalama vilitumia mabomu ya machozi kuwashambulia waandamanaji.

Sheria hiyo, iliyopitishwa na bunge Julai 26, inaweka ulazima wa chanjo ya kwa wafanyikazi wa hospitali, wauguzi na wazima moto.

Sheria inahitaji ombi la hati ya Covid-19, ambayo inahitaji kuweka kumbukumbu ya chanjo kwenye mlango wa sehemu za shughuli na kumbi mbalimbali ili kuonyesha matokeo ya vipimo vya PCR katika saa 48 au kuthibitisha kuwa mgonjwa ameugua na kupona miezi sita iliyopita.

Pia, pamoja na sehemu za hafla za ushiriki mkubwa kama matamasha, migahawa, usafiri wa umma na sehemu za ndani zilizo na uwezo wa kubeba zaidi ya watu 50 pamoja na kumbi za burudani.

**TRT**



# Brazil vs Mexico nusu fainali Olimpiki

**TOKYO, Japan**

TIMU ya Brazil ipo kwenye nafasi nzuri ya kushinda medali ya dhahabu kwa mara ya pili mfululizo kwenye michezo ya Olimpiki baada ya kuifunga Misri 1-0 na kutinga nusu fainali.

Bao la kipindi cha kwanza kutoka kwa Matheus Cunha liliwawezesha mabingwa hao watetezi kutinga kwenye nusu fainali hiyo ambapo sasa watacheza na Mexico, kesho Jumanne.

Wenyeji wa mashindano hayo Japan watacheza na Hispania katika hatua hiyo.

Japan wametinga hatua hiyo baada ya kuwafunga New Zealand 4-2 kwa changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya kutoka suluhu dakika 90 na za nyongeza, huku Hispania ikiwatoa Ivory Coast 5-2 katika muda wa ziada.


Wakati Max Gradel alipoiweka Ivory Coast 2-1 mbele katika dakika ya kwanza ya muda wa nyongeza, walionekana kama wanakwenda nusu fainali.

Lakini straika wa Wolves, Rafa Mir akasawazisha baada ya kuugusa mpira kwa mara ya kwanza akitokea benchi, halafu akafunga mara mbili kwa Hispania kuiwezesha kutinga nusu fainali kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 21.

Wakati mchezo huo ulizalisha mabao saba, kwenye mchezo wa Mexico dhidi ya Korea Kuisni ilitengeneza mabao tisa - baada ya kuibuka na ushindi wa 6-3 na sasa itacheza nusu fainali na Japan.

Japan wapo kwenye nafasi nzuri ya kushinda medali yao ya kwanza kwenye soka katika michezo ya Olimpiki tangu walipopata ya shaba kwa mara ya kwanza mwaka 1968.

# WAWAKILISHI WA NIGUEZ WAPAA ENGLAND



**MADRID, Hispania**

WAWAKILISHI wa nyota wa Atletico Madrid, Saul Niguez jana Jumapili walipaa kulekea England kwa ajili ya kufanya makubaliano na wateja wao kwenye Ligi Kuu, Liverpool na Manchester United ambazo wanawania huduma ya mchezaji huyo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 amepewa ruhusa ya kuondoka kwa mabingwa hao wa Hispania kipindi hiki cha majira ya joto.

Atletico wana matumaini ya kuingiza fedha kwa mauzo ya Saul kipindi hiki na wamewapa ruhusa wawakilishi wao kutafuta klabu mpya kwa ajili ya kiungo huyo.

Na kwa mujibu wa Mirror, jana Jumapili walisafiri kwenda England ili kufikia makubaliano na klabu ya Ligi Kuu.

Saul mwenyewe ana matumaini kwamba, majaliwa yake yatafikiwa hivi karibuni, na hataki kutafuta klabu mpya wakati msimu utakapokuwa umeanza.

Kiungo huyo amekuwa mchezaji muhimu kwa kikosi cha Atleti akicheza zaidi ya mechi 300 kwa Los Rojiblancos hao.

Alicheza mechi 33 za LaLiga msimu uliopita, akifunga mabao mawili kwa Atletico wakati wakishinda taji lao la kwanza tangu mwaka 2014.

# Chelsea kupunguza ada ya Abraham

**LONDON, England**

CHELSEA inajiandaa kupunguza thamani ya Tammy Abraham huku Arsenal, West Ham na Aston Villa zikiwa zinamwania ambapo ada yake ya sasa inatajwa kuwa ni pauni milioni 40.

Blues hao wanajaribu kutafuta fedha wakati wakiwa na nia ya kutaka kukamilisha uhamisho wa Erling Haaland.

Mtandao wa 90min.com mwanzoni mwa mwezi uliopita ulibainisha kwamba, Roman Abramovich yupo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 150 kumsajili fowadi huyo, licha ya Dortmund kuonesha kutokuwa na nia ya kumuuza kipindi hiki cha majira ya joto.

Chelsea imekuwa ikiangalia uwezekano wa kuwauza baadhi ya wachezaji wake ili kupata fedha za kuwanunua wengine wapya, huku Fikayo Tomori na Marc Guehi tayari wakiwa wameshauzwa.

Na sasa klabu hiyo inajiandaa kumuuza Abraham ili kuongeza fedha kwenye usajili wao.

Nyota huyo wa kimataifa wa England amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England ikiwamo Arsenal, West Ham na Aston Villa.

Lakini hakuna kati ya hizo ambayo ipo tayari kutoka kiasi cha pauni milioni 40 kinachotakiwa na Chelsea, na sasa gazeti la Sun limeripoti kuwa Blues hao wapo tayari kupunguza bei.

Ripoti hiyo inasema kuwa klabu hiyo ya London ipo tayari kupunguza bei kwa pauni milioni 5 ili klabu zinazomtaka ziweze kumsajili.

## HABARI MICHEZO




# KOEMAN

## ASIFIA UPATINA WA DEPAY, GRIEZMANN

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amefurahishwa na muunganiko wa Memphis Depay na Antoine Griezmann wakati Barcelona ikibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Stuttgart, Jumamosi.

Barca waliendeleza rekodi nzuri kwenye mechi za maandalizi ya msimu mpya, ikishinda zote tatu katika dimba la Mercedes-Benz Arena.

Depay, ambaye alijiunga na mi-amba hao wa LaLiga kwa uhamisho huru Juni baada ya kuondoka Lyon, alianza kufunga dhidi ya timu hiyo ya Bundesliga dakika ya 21.

Raia huyo wa Uholanzi alipokea krosi kutoka kwa Frenkie de Jong akiwa aneo la boxi, kabla ya kumvisha kanzu Pascal Stenzel na kupiga shuti lililomshinda golikipa Fabian Bredlow.

Halafu Depay akawa na mchango mkubwa kwa bao la pili la Barca lililofungwa dakika 15 baada ya kwa kumpasia kwa kisigino Griezmann aliyempa kinda Yusuf Demir na kufunga.

Na mara baada ya mchezo huo, Koeman alisifia upatina wa wawili hao.

"Kwa uhakika watu wanajua kuhusu Memphis," alisema.

"Amekuwa kule (Manchester) United, na miaka michache iliyopita Lyon na juu ya yote, ameonesha kuwa ni mfungaji mzuri zaidi."

## JUVENTUS INAJIAMINI KUMSAJILI LOCATELLI

**TURIN, Italia**

JUVENTUS inajiamini kumsajili Manuel Locatelli kutoka Sassuolo baada ya kuweka mezani ofa ombayo makamu wa rais, Pavel Nedved ameilezea kuwa ni "ofa sahihi."

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23 amejiimarisha yeye mwenyewe akiwa kule Sassuolo kwa kipindi cha misili miwili akicheza kwenye Serie A na sasa anawaniwa na klabu kadhaa Ulaya.

Locatelli alikuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kwenye michuano Euro 2020, wakati Italia ikitwaa ubingwa huo kwenye fainali dhidi ya England, na alifunga mabao mawili dhidi ya Uswisi kwenye hatua ya makundi.

Arsenal tayari ilipeleka ofa yake kwa ajili ya kiungo huyo, huku wapinzani wao kwenye Ligi Kuu ya England, Liverpool pia wamehusishwa nae, lakini Nedved ana uhakika kwamba, Juve itashinda mbio za kumsajili nyota huyo.



"Tumezungumza na Sassuolo na tumetoa ofa yetu, ambayo tunaamini ni sahihi kwa hali ya sasa, hasa kutokana na namna soko usajili lilivyoathiriwa na mlipuko wa ugonjwa wa COVID," alisema Nedved akiiambia Sport Mediaset.

"Tunajiamini kwamba hii ni ofa nzuri na tunashawishika kuwa ni ofa sahihi kwa sasa, kwani kwa kawaida kuna mambo ambayo lazima yajadiliwe na kukamilishwa.

"Wakati unapomtaka mchezaji na mchezaji anakutaka, hilo jambo la kawaida kuweka majadiliano mbele."

# VILLA YATHIBITISHA KUMSAJILI BAILEY

**LONDON, England**

ASTON Villa imethibitisha kufikia makubaliano na Bayer Leverkusen kwa uhamisho wa Leon Bailey.

Villa ipo kwenye harakati za usajili huku nahodha wake, Jack Grealish akiripotiwa kuwa kwenye rada za Manchester City ambao wametoa ofa ya pauni milioni 100 kutaka kumsajili.

Hata hivyo, wakati dili la Grealish - ambaye ameripotiwa kupewa ofa ya mkataba mpya na Villa -kocha, Dean Smith anapanga kuimarisha safu yake ya ushambuliaji kwa kumwongeza, Bailey.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Jamaica, Bailey alifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho 10 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, katika Klabu ya Leverkusen kwenye mechi 40 za mashindano yote msimu huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye alijiunga na Leverkusen kutoka Klabu ya Ubelgiji ya Genk mwaka 2017, atasaini mkataba wa kujiunga na Villa mara baada ya kukamilisha vipimo vya afya yake, kwa mujibu wa taarifa ya tovuti ya klabu hiyo.

Hakuna tarifa zaidi zilizoripotiwa, ingawa inadaiwa kwamba, Leverkusen wanataka kiasi cha pauni milioni 30 ili kumwachia Bailey.

Dili hilo likikamilika, Bailey atakuwa mchezaji wa tatu wa Villa kusajiliwa kipindi hiki cha dirisha la uhamisho wa majira ya joto, baada ya kusajiliwa kwa Emiliano Buendia na Ashley Young.



## KWA UFUPI

**BELLERIN CHAMBO KWA MARTINEZ**
ARSENAL inafikiria kumtumia beki wake, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 26 kama chambo ya kumpata mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 23, huku Tottenham Hotspur pia ikiwa mbioni kutaka kumsajili straika huyo wa Argentina iwapo watamuuza Harry Kane mwenye miaka 28. ***(Athletic)***

**VILLA KUMUUZA GREALISH**
ASTON Villa iko tayari kukubali dau la Manchester City la pauni milioni 100 ili kumuuza kiungo wa kati, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports)***

**CANTWELL AWANIWA VILLA**
KOCHA wa Aston Villa atawasilisha ombi la kumsajili kiungo wa kati wa Norwich na England, Todd Cantwell mwenye umri wa miaka 23, iwapo Jack Grealish ataondoka hapo Villa Park. ***(Express)***

**PROWSE DAU LA PILI**
ASTON Villa pia inatarajiwa kuwasilisha ombi la pili la kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Southampton, James Ward Prowse baada ya dau la kwanza la pauni milioni 25 kukataliwa ***(Mail)***

**HAALAND BADO AWINDWA MAN**
MANCHESTER United ina matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21, msimu ujao na wanaamini kwamba, uhusiano wake na kocha, Ole Gunnar Solskjaer huenda ukachangia kwa kuwa mchezaji huyo ni raia wa Norway sawa na kocha huyo. ***(Star)***

**GOURNA-DOUATH AGOMBEWA**
CHELSEA inakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa Atalanta, Bayer Leverkusen na Borussia Dortmund katika mbili za kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa na klabu ya St. Etienne, Lucas Gourna-Douath, ambaye atakuwa na umri wa miaka 18 kufikia wiki hii. (RMC Sport)

**NIGUEZ ANUKIA EPL**
WAWAKILISHI wa kiungo wa kati wa Atletico Madrid na Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26 wataelekea England leo Jumatatu ili kujadiliana kuhusu uhamisho wa mchezaji huyo, huku klabu za Manchester United na Liverpool zikimtafuta nyota huyo. ***(Mirror)***


**SHAW KUPEWA MKATABA**
MANCHESTER United inajianda kumpatia Luke Shaw mkataba mpya baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kuonesha kiwango kizuri wakati alipokuwa anaichezea England kwenye michuano ya Euro 2020. ***(Mail)***

**ROMERO AOTA MBAWA SPURS**
JUHUDI za Tottenham Hotspur kutaka kumsajili beki wa Argentina mwenye umri wa miaka 23, Cristian Romero kutoka Atalanta zimegonga mwamba, baada ya awamu ya mwisho ya mazungumzo kati ya klabu hizo mbili kukamilika bila makubaliano. ***(Gianluca Di Marzio)***

**STONES NA MKATABA**
MLINZI wa Manchester City, John Stones mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kupatiwa mkataba i mpya, lakini mazungumzo ya kuongezea winga, Raheem Sterling yamegonga mwamba. ***(Mirror)***

**SOARES ATAKIWA FENERBAHCE**
KLABU ya Fenerbahce inafikiria kumsaini beki wa Ureno na Arsenal, Cedric Soares mwenye umri wa miaka 29. ***(Fotomac)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANE ADHAMIRIA KUTUA MAN CITY

**Ashafanya maamuzi juu ya majaliwa yake na anataka kujiunga na Grealish kwa mabingwa hao**

**LONDON, ENGLAND**

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Harry Kane amedhamiria kujiunga na Manchester City kipindi hiki cha majira ya joto, akitumaini kuungana na mchezaji mwenzake wa timu ya taifa ya England, Jack Grealish pale kwenye dimba la Etihad.

Uwezekano wa Grealish kuondoka Aston Villa uliongezewa nguvu zaidi Jumamosi, baada ya klabu hiyo kutangaza kumsajili winga wa Bayer Leverkusen, Leon Bailey ambaye anaonekana kuwa kama ndiye mrithi wa nahodha huyo.

Na gazeti la Telegraph limeripoti kwamba, Kane pia tayari ameshafanya maamuzi juu ya majaliwa yake, na sasa anasukuma uharaka wa yeye kuondoka Spurs kipindi hiki cha majira ya joto kujiunga na Grealish kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ameshaweka wazi hadharani mpango wake wa kutaka kuondoka kule London Kaskazini, akibainisha pia katika mahojiano yake aliyofanya na Gary Neville.

Kane alielezea kwamba, anataka kushinda mataji katika maisha yake ya uchezaji, na atakaa chini kuzungumza na mwenyekiti, Daniel Levy kujadiliana kuhusu hilo.

Nahodha huyo wa England na Tottenham anaonekana sasa amefikia maamuzi yake, na anasubiri uhamisho wa kwenda Man City, ambako atakuwa na nafasi bora zaidi ya kushinda mataji.

Mtandoa wa 90min.com hivi karibuni ulibainisha kwamba, Spurs haikuwa na mpango wa kumuuza Kane kipindi hiki cha majira ya joto, licha ya presha kubwa kutoka kwa wapinzani woa hao wa Ligi Kuu England.

Hata hivyo, Kane bado anasubiri maamuzi ya Levy na anajiamini kuwa uhamisho wake utafanikiwa kipindi hiki.

Tottenham wanaweza kutaka kiasi kikubwa zaidi cha fedha, hasa ikizingatiwa kwamba, fowadi huyo mkataba wake wa sasa umebakiwa na miaka mitatu kumalizika.

HABARI MICHEZO

# SHUGHULI PEVU DSTV MSIMU MPYA WA SOKA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya MultiChoice Tanzania imezindua kampeni ya msimu mpya wa soka ijulikanayo kama Biriani Iendelee na kuwataka Watanzania wakae mkao wa kula kabla ya kuanza kwa mtifuano wa Ligi Kubwa duniani kupitia DStv.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo alisema Tanzania haijaachwa nyuma kwenye joto la soka ambalo limeanza kufukuta kote ulimwenguni, kwani zimebaki siku chache tu kabla ya kuanza mtifuano wa ligi kubwa duniani.

Alisema mashabiki wa soka hapa nchini watashuhudia Premier League (Uingereza), LaLiga (Hispania) na Serie A (Italia) mbashara kupitia DStv.

Alisema pia kunogesha zaidi utamu wa burudani ya soka, wanazi wa soka nchini pia wataungana na wenzao kote duniani kushuhudia michuano maarufu ya UEFA Europa Ligi inayorudi rasmi ndani ya DStv, na msimu huu michuano hii itakuwa ikipatikana kupitia DStv pekee.

"Burudani ndani ya DStv ni bandika bandua, paukwa pakawa. Kwani wakati michuano maarufu ya Olympics ikielekea ukingoni, wateja wa DStv wataendelea kuchekelea kwani kuanzia Agosti 7, michuano ya ligi hizi maarufu duniani itaanza kutimua vumbi kwa mechi ya Ngao ya Jamii kati ya Leicester City dhidi ya Manchester City ikionyeshwa mbashara kupitia DStv pekee," alisema Shelukindo. "Kama kawaida ya DStv, wateja wake hawana sababu ya kuwa wanyonge, kwani ligi zote kubwa sasa zipo ndani, hapa ni bandika bandua, chomoa chomeka burudani juu ya burudani," aliongeza.

Shelukindo alisema mbali na kuwapo kwa michuano ya UEFA Europa ndani ya DStv pekee, Watanzania pia wataendelea kufurahia Ligi Kuu ya Uingereza ambayo itakuwa ikitangazwa kwa lugha ya Kiswahili na watangazaji nguli wa soka hapa nchini.

"Manjonjo yetu katika kukuletea matangazo mbashara ya Ligi Kuu ya Uingereza sasa yameongezwa kwani tumeongeza wachambuzi na watangazaji wa Kiswahili."

Alisema wateja wa DStv wa kifurushi cha Compact, Compact Plus na Premium watashuhudia mechi zote za Premier League, LaLiga, Serie A na UEFA Europa League. Wateja wa vifurushi vya Bomba na Family watashuhudia mechi zote za LaLiga, Serie A na baadhi ya mechi za Premier league.

"Mteja wetu wa kifurushi cha Bomba cha 19,900 atashuhudia mechi zote 380 za LaLiga, mechi zaidi ya 100 za Seria A na mechi zaidi ya 100 za Premier League wakati wateja wa kifurushi cha Family 29,900 watashuhudia mbashara mechi zote 380 za Serie A, mechi zote 380 za Serie A na mechi 100 za Premier League."

Msimu huu wa soka utashuhudia patashika nguo kuchanika kwani kwenye Premier League, Pep Guardiola wa Manchester City atataka kudumisha umwamba wake kitu ambacho vigogo wa ligi hiyo kama Liverpool, Chelsea na Manchester United hawawezi kukubali kirahisi.

Hispania nako kutawaka moto kwenye LaLiga, ambapo kwa kuanzia, Atletico Madrid haitakubali kuwa kwa Real Madrid na Barcelona na njaa ya ushindi ya Sevilla msimu huu itaongeza utamu.

Kule Serie A vijogoo kama Juventus, AC Milan, Napoli, Lazio na AS Roma hazitakuwa tayari kumuacha Inter Milan atambe tena.




Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo (katikati), akikabidhi kombe kwa timu ya TASWA baada ya kuibuka washindi katika bonanza maalum la DStv kuzindua msimu mpya wa soka. Bonanza hili lilihusisha timu zilizoundwa na maveterani wa soka hapa nchini ambao ni mashabiki wa Arsenal, Man U na Liverpool. Bonanza hilo lilifanyika jijini Dar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Green Warriors wapania kupanda Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Green Warriors, umeweka wazi kwamba msimu 2021/22 watahakikisha wanatimiza ndoto zao za kupandisha timu yao na kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2022/23.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makamu Mwenyeikiti wa Green Warriors, Muharami Hali, alisema baada ya kupambana muda mrefu kushindwa kucheza Ligi Kuu sasa wamejizatiti na kuweka mipango vizuri kwa ajili ya kufanya vizuri katika ligi daraja la kwanza.

Alisema katika kuhakikisha wanakwenda kufanya vizuri wanasajili wachezaji wenye uzoefu wa kutosha, kwa lengo la kuboresha kikosi cha timu yao kwa ajili ya msimu mpya wa daraja la kwanza.

"Tutafanya maboresho katika kikosi cha timu yetu, kusajili wachezaji wazoefu na watakaotusaidia na kufanya vizuri kwenye michezo yetu ya ligi daraja la kwanza wa msimu wa 2021/22 na baadaye kupanda na kucheza Ligi Kuu msimu wa 2022/23," alisema Muharami.

Alisema kuhusu benchi la ufundi litaendelea kuongozwa na Kocha Mkuu, Grayson Haule na huku wakisubiri ratiba kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa lengo la kufahamu kituo watakachopangiwa.

Alisema safari hii hawataki mchezo na kuhakikisha wanaboresha timu yao ili kufikia malengo hayo ya kufanya vizuri kwa msimu huu wa 2021/22 na kurejesha makali yao ya awali.

# Geita Gold wajipanga uwekezaji na usajili

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Geita Gold FC, George Mbiligeda, amesema wameanza uwekezaji kwa kusajili wachezaji wapya kwa lengo la kuboresha timu yao pamoja na miundombinu ya uwanja watakaotumia katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mbiligeda alisema wanashirikiana na uongozi wa mkoa huo kuhakikisha wanafanya ukarabati mzuri wa uwanja wa Magogo ambao utakuwa ni uwanja wao wa nyumbani.

Alisema wakati viongozi wakiendelea na suala la miundombinu pia kuna kamati ya usajili wameiunda kwa lengo la kufuatilia wachezaji ambao wamependekezwa na benchi la fundi.

**"Tayari tumeanza kufanyia kazi mapendekezo ya usajili, kipaumbele chetu ni kusajili wachezaji wazawa na wenye viwango vya juu kwa sababu tuna hitaji kushindana kwenye Ligi Kuu na sio kwenda kushiriki kwa msimu unaofuata tunarudi chini," alisema.**

Aidha, alisema kutakuwa na mabadiliko kidogo kwenye benchi la ufundi kwa sababu wanahitaji kuimarisha benchi hilo pamoja na kikosi hicho ili kuleta ushindani mkubwa kwa timu za ligi hiyo.

Alisema watakapo kamilisha suala la usajili na kuingia mapema na kuanza maandalizi rasmi ya msimu mpya wa ligi hiyo.

Michezo
Jumatatu Agosti 2, 2021
Nipashe



## Kane adhamiria kutua Man City

HABARI UK. 22



Nyota wa Timu ya Taifa ya Brazil chini ya umri wa miaka 23, Gabriel Jesus (katikati), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Misri wakati wa mchezo wa robo fainali kwenye michezo ya Olimpiki baina ya timu hizo juzi, Tokyo, Japan. Brazil ilishinda bao 1-0 na kufuzu nusu fainali itakayopigwa Jumanne dhidi ya Mexico. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, AZAM ZAFUNIKA USAJILI, SIMBA KIMYA

## ●●●Vifaa vya Jangwani kuonekana kombe la Kagame, Dewji asema usajili wao ni siri kwani...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha la usajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu ukiwa umefunguliwa, huku mwisho wa kupeleka majina ya wachezaji Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ukiwa Agosti 15, klabu za Yanga na Azam FC zimeonekana kuanza usajili kwa nguvu, huku Mabingwa Watetezi Simba wakiwa kimya.

Tayari Azam imeshafanya usajili wa wachezaji wapya sita, watano wakiwa ni wa kigeni na mmoja Mtanzania, huku Yanga ikimshusha straika kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Fiston Mayele.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kuwa wanachama na mashabiki wa Yanga watarajie kuwaona wachezaji ambao wamewasajili na wanaotarajia kuwasajili, kwenye michuano ya Kombe la Kagame lililoanza jana nchini.

"Mayele, tayari ametua na Djuma Shaaban tumemalizana naye kwa asilimia 90, ukikamilika tutawaambia," alisema.

Habari za ndani za klabu hiyo zinasema kuwa mbali na Mayele, pia Yanga iko kwenye mazungumzo na kiungo kutoka Msumbiji, Jimmy Ukonde.

Wachezaji wengine ambao wapo kwenye mazungumzo na Yanga ni Dickson Ambundo wa Dodoma Jiji na Yusuph Athumani wa Biashara United.

Kwa upande wa Azam, timu hiyo ilimshusha straika Idris Mbombo kutoka El Gouna ya Misri kwa mkataba wa miaka miwili.

Huyo anakuwa ni straika wa pili kwa Azam, ambapo mwanzo ilimsajili Rodgers Kola raia wa Zambia.

Wapo viungo, Wazambia, Charles Zulu, Paul Katema na Mkenya Kenneth Muguna, huku ikimsajili mchezaji Mtanzania, Edward Manyama kutoka Ruvu Shooting.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat' amesema kuwa zoezi la usajili bado linaendelea, lakini sasa linahamia kwa wachezaji wa ndani.

"Zoezi letu linaendelea, baada ya kusajili kimataifa, sasa tunageukia usajili wa ndani," alisema.

Wakati hali ikiwa hivyo kwenye klabu za Yanga na Azam, ukimya umetawala kwenye klabu ya Simba kwenye masuala ya usajili.

Mpaka sasa klabu hiyo haijatangaza kusajili mchezaji yoyote, ingawa kumekuwa na tetesi ambazo hata hivyo hazina nguvu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Simba, Mohamed Dewji, wakati akitambulisha kuweka fedha za uwekezaji kiasi cha Sh. bilioni 20, alisema kuwa inafanya siri kubwa kwenye usajili wake kwa sababu inagombea pamoja na klabu kubwa barani Afrika.

"Simba kwa sasa ni timu kubwa, usajili wetu tunaufanya kuwa siri kwa sababu tunagombea wachezaji wa klabu kubwa Afrika zenye pesa nyingi. Kwa hiyo tunafanya siri. Lakini tutasajili na tutawatangazia tukikamilisha," alisema Dewji.

## Mbombo aahidi mabao Azam

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA mpya wa Azam FC, Idris Mbombo amewataka mashabiki wa Azam FC kujitokeza kwa wingi pale timu yao itakapocheza kwa sababu watakuwa na furaha na hatowaangusha.

Akizungumza kwa mara ya kwanza baada ya kusajiliwa na Azam Jumamosi kwa mkataba wa miaka miwili akitokea El Gouna ya Misri, Mbombo amesema kuwa anajisikia vizuri kutua Azam kwa sababu ni klabu ambayo anaifahamu.

**"Namshukuru Mungu kwa kusaini Azam. Najisikia vizuri, naifahamu Azam na natumaini nitafanya vizuri. Nawaambia mashabiki wa klabu hii wawe wanakuja kwa wingi uwanjani kutu sapoti timu yao. Mimi nitacheza kwa bidii na kwa neema ya Mungu kila kitu kitakwenda vizuri," alisema straika huyo.**

Mbombo, ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo ameingia mkataba wa miaka miwili mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam Abdulkarim Amin 'Popat', utakaomfanya kuhudumu ndani ya timu hiyo hadi mwaka 2023.

Straika huyo amewahi kuzichezea kwa mafanikio makubwa klabu za Nkana Red Devils na Kabwe Warrios zote za Zambia.

Usajili wa mchezaji huyo ni mfululizo wa klabu ya Azam FC kufanya maboresho makubwa kwenye kikosi chao kuelekea msimu ujao ambapo itacheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Tayari, Azam imeshawatia kibindoni wachezaji kama Charles Zulu, Paul Katema na Rodgers Kola, wote ni Wazambia, Mkenya Kenneth Muguna na beki wa kushoto mzawa, Edward Many-

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9

9 770856 541002 >